# Nipashe

Ijumaa Aprili 16, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580552

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**TCRA** yawatuliza watumiaji wa simu gharama vifurushi

UKURASA 3



**HATIMA** vita vya urais wa TLS leo, serikali yatoa neno

UKURASA 3

# Shehena ya mafuta kula yatua Dar



Kinamama wakichagua nazi katika Soko la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana, bidhaa inayotumika zaidi kwa maandalizi ya futari hasa katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. **Picha ndogo:** Wananchi wakichagua mihogo katika Soko la Buguruni jijini humo jana. **PICHA: MIRAJI MSALA/JUMANNE JUMA**



## Pius Msekwa amchambua Rais Samia-2



UK. 19

## Waziri atoa msimamo wa vibali vya kazi kwa wageni

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Hivi ndivyo wananchi wanavyoibiwa gesi

UK. 4

MICHEZO SIMBA : TUMEONYESHA UKUBWA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Katambi atoa msimamo vibali vya kazi kwa wageni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Patrobasi Katambi, amewaomba waajiri, wawekezaji na waombaji wote wa vibali vya kazi kufika katika ofisi ya Idara ya Kazi ili waweze kupewa utaratibu sahihi wa kuomba vibali hivyo.

Pia, amewaagiza maofisa kazi kubadilika katika utendaji wao huku akiwataka kusimamia vyema taratibu na sheria za kazi kwa kulinda maslahi ya wafanyakazi na kuacha kuwa vibaraka wa waajiri.

Naibu waziri huyo aliyasema hayo juzi wakati wa kikao kazi na maofisa kazi waliopo Idara ya Kazi Makao Makuu Dodoma, Mamlaka ya EPZA na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Kikao hicho kilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, aliyoyatoa wakati wa kikao na Menejimenti ya Ofisi hiyo Aprili 9, mwaka huu.

Akizungumzia kuhusu mfumo wa kielektroniki wa vibali vya kazi kwa wageni, alisema hivi karibuni Ofisi ya Waziri Mkuu itazindua mfumo huo ili wahusika waweze kuomba vibali hivyo kwa njia ya mtandao (online) hatua itakayosaidia kupunguza urasimu.

"Mfumo wa kielektroniki wa vibali vya kazi utachangia kurahisisha utoaji huduma hususan katika kushughulikia maombi ya vibali, pia utaongeza ufanisi kiutendaji kwenye idara ya Kazi.

"Maagizo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais yanatutaka tuhakikishe kibali kinatolewa ndani ya siku 14 na kisivuke siku hizo, hivyo hakikisheni mnatoa majibu ya vibali kwa wakati mara tu baada ya kuyapokea," alisema.

Alitaja baadhi ya upungufu ikiwamo baadhi ya waajiri wanaopaswa kuwaombea vibali wafanyakazi wao kuwa na tabia ya kutumia mawakala au madalali kufuatilia vibali vya kazi jambo ambalo limekuwa na sura tofauti kutokana na kuwatozwa fedha hali inayosababisha udanganyifu mkubwa na kutia doa ofisi.

"Vishoka hao wamekuwa wakienda kwa mwajiri na kuanza kuwadanganya hapa kuna hili unajua huna sifa kwa hiyo inabidi tuliweke vizuri suala lako, wakati akidanganya hivyo kwa waajiri, kishoka huyo ofisini anafuata taratibu zilezile kule mwajiri anaamini kwamba ili upate lazima kuwe na fedha matokeo yake inaoneka huku kuna rushwa, sasa nitoe onyo tutachukua hatua kali kwa watu wanaojifanya kuhusika na vibali vya kazi," alifafanua.

Kadhalika, alisema uwapo wa baadhi ya watumishi wanaofanya kazi kwa mazoea kutokana na kukaa muda mrefu katika kituo cha kazi kunasababisha kutengeneza mtandao mkubwa na watu wengine hali inayosababisha baadhi yao kuanza kutengeneza mianya ya rushwa.

Alisema kuwa maofisa ambao wanaojihusisha na vitendo hivyo watachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kuwabadili vituo vya kazi. "Nina mifano ya vibali vingi watu wanalalamika wanakuja kuomba vibali anaambiwa njoo kesho njoo kesho, kumbe kibali kimeshaenda kwa kamishna na uamuzi ameshatoa, lakini kunatengenezwa mazingira ya sintofahamu na maofisa wasio waaminifu, tutawapangua kweli kweli."

Kamishna Msaidizi wa Kazi, Andrew Mwalwisi, aliahidi kuwa Idara ya Kazi itatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa kwa weledi na uadilifu. Alisema hali hiyo itasaidia kuondoa malalamiko yanayotolewa na wadau kwa maofisa kazi nchini.

Alisema kuwa uwajibikaji wa kuridhisha wa maofisa kazi katika maeneo yao waliyopangiwa, utarahisisha utatuzi wa changamoto ya wafanyakazi na kupunguza malalamiko ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa waajiri kutambua wajibu wao kwa wafanyakazi.

"Malalamiko yakiwa mengi ni ishara kwamba afisa kazi wa eneo husika hafanyi kazi vizuri, unakuta mfanyakazi anasimamishwa kazi bila sababu ya msingi "unfair termination" halafu afisa kazi huchukui hatua zozote wala hutoi maelekezo ya hatua zipi zinapaswa kuchukuliwa, hiyo ni wazi kuwa hufai kuwapo katika nafasi hiyo.

"Lakini kama unakuwa na utaratibu wa kuwatembelea wafanyakazi katika maeneo yao ya kazi na unahakikisha vyama vya wafanyakazi katika maeneo yao ya kazi viko imara na ofisa kazi uko imara, waajiri watakuwa wanafuata sheria na taratibu," alisema Katambi.

Alisema Februari 26, mwaka huu, Waziri Mhagama alizindua Mpango kazi wa kushughulikia malalamiko na kero za wafanyakazi, waajiri na wadau wengine katika sekta ya kazi na ajira lengo likiwa kushughulikia kwa urahisi matatizo yao na pia kuhakikisha migogoro inatatuliwa haraka pamoja na kusimamiwa kwa maslahi yao.

"Uwepo wa mpango huu wa kusikiliza na kushughulikia malalamiko ya wadau katika sekta ya kazi na ajira (Labour Clinic), ambao unatekelezwa kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi kwenye mikoa itapunguza gharama na muda unaotumiwa na wadau hao katika kushughulikia na kufuatilia malalamiko yao na kuwapa muda zaidi kuendelea na kazi za kujenga uchumi wa taifa," alisema.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi (wa tatu kushoto), akizungumza na maofisa kazi wa idara ya kazi makao makuu Dodoma, Mamlaka ya EPZA na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), juzi. Kushoto kwake ni Kamishna Msaidizi wa Kazi, Lilian Francis. **PICHA: PAUL MABAEJA**

# Shehena mafuta ya kula yatua Dar

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAKATI bei ya mafuta ya kula inaendelea kuripotiwa kupanda katika mikoa mbalimbali nchini, serikali imesema meli mbili zimewasili nchini zikiwa na shehena ya mafuta hayo.

Katika mahojiano maalum na Nipashe kwenye Viwanja vya Bunge jijini Dodoma jana, Waziri wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo, alibainisha kuwa meli ya kwanza ilianza kushusha mzigo juzi kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

"Kwa sasa kuna meli mbili zinashusha shehena. Kwa hiyo, tunaamini wiki hii tutakuwa na mafuta ya kutosha. Moja ilianza kushusha jana (juzi) na nyingine itaanza ushusha tarehe 29 (Aprili 29).

"Kwa hiyo, hizo (meli) zikishusha, tutakuwa na mafuta mengi kwenye soko na bei za mafuta ya kula itashuka," aisema Prof. Mkumbo.

Nipashe ilipotaka kufahamu mikakati ya serikali kukabiliana na uhaba wa mafuta na sukari nchini kunakosababisha bei za bidhaa hizo kupanda kwa kasi, waziri huyo alianika mkakati ambao mbali na mambo mengine, unahusisha kuweka bei elekezi kwenye mazao muhimu nchini.

"Serikali inaweka bei elekezi. Kwa mfano, kule Dar es Salaam bei elekezi ya sukari ni Sh. 2,600 kwa kilo. All the time (muda wote) tunawakumbusha wafanyabiashara kwamba wazingatie hicho kiwango.

"Lakini, kwenye mambo ya biashara katika ulimwengu wa leo, kuna kitu kinaitwa soko huria. Kwa hiyo, serikali haiwezi kuingilia sana kwa sababu itaharibu soko.

"Kazi ya serikali ni kuhakikisha kwamba inaangalia wale watu ambao ni wanyonge wasije wakaumia, lakini pia wafanyabiashara wasitumie nafasi yao au fursa, mfano huu Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, kupandisha bei.

"Kwa hiyo, hilo ndilo kubwa tunalolifanya -- kuongea nao, kuwasisitiza na kuwakumbusha, na pale ambapo panahitajika sheria, tunatumia sheria. Kwa sasa tuna zao moja tu la sukari ambalo limewekewa bei elekezi na serikali, mazao mengine hayana.

"Sasa tunavyokwenda hivi tunaona kuna matatizo haya (uhaba wa mafuta na sukari), (wafanyabiashara) wanaifanya serikali ifikirie kuwa na bei elekezi kwenye kila zao, hasa kwenye mazao yale ambayo ni muhimu kama vile mafuta, mchele, sukari.

"Lakini, hicho ni kitu cha mwisho ambacho serikali inafikiria kufanya ili kudhibiti soko na kukabiliana na uhaba wa bidhaa hizo muhimu kwa wananchi," alisema.

**UTAPELI WAKITHIRI**

Mbali na bidhaa hiyo kuwa adimu, pia kumeibuka utapeli kwa baadhi ya watu kuuza mafuta kwa njia ya udanganyifu.

Akizungumza na Nipashe mmoja watu waliowahi kutapeliwa (jina limehifadhiwa) alisema alinunua ndoo tatu za mafuta zenye ujazo wa lita 10 kila moja, lakini alipozingua ndani alikuta kumejazwa maji machafu.

Kijana huyo alieleza kwamba: "Alikuja mtu kwenye eneo langu la biashara akasema anauza mafuta ya kula kwa bei nzuri, aliniambia anauza mafuta ya kula lita tano kwa Sh. 25,000 badala ya Sh. 35,000".

Aliongeza: "Nikamwambia anietee ndoo nane lakini baadaye nikabadilisha nikamwambia anieletee ndoo tatu, nikampa Sh. 70,000, Sh. 5,000 nikamwambia ni punguzo, nikazichukua ndoo zikiwa zimebanwa, kuziweka ndani, siku ya tatu nilipozifungua nikakuta ndoo zote zimejazwa maji machafu yakiwa na matakataka".

**HALI ILIVYO KWA SASA**

Nipashe lilipita katika baadhi ya maeneo na kukuta bei ya mafuta ya kula ikiwa iko juu.

Katika uchunguzi huo ilibainika kwamba bei ya bidhaa hiyo imeongezeka kuanzia Sh.1, 000 hadi 10,000 kutegemea na ujazo wa mafuta.

Katika Jiji la Dar es Salaam mafuta ya Alizeti yenye ujazo wa lita tano yanauzwa Sh. 30,000.

Wilaya ya Moshi mafuta safi ya lita 20 yamepanda kutoka Sh. 67,000 hadi Sh. 70,000. Ujazo wa lita 10 kutoka Sh. 33,000 hadi Sh. 35,000. Mkoani Manyara, dumu la lita 20 linauzwa Sh.68,000 kwa bei ya rejareja huku dumu la lita tano likiuzwa Sh. 17,000.

Visiwani Zanzibar galoni ya lita 20 la mafuta ya kula linauzwa Sh.55,000 badala ya Sh.35,000 na lita moja ya mafuta hayo inauzwa Sh.5,000 badala ya Sh.4,000.

Mkoa wa Pwani eneo la Maili moja, lita moja inauzwa Sh.4,500 kutoka Sh.3,000, lita 10 inauzwa Sh.35,000 kutoka Sh.31,000, mafuta ya alizeti lita moja imefikia Sh. 4,500 hadi Sh. 5,000, huku lita tano ikiuzwa Sh.20,000 hadi Sh.25,000 awali ilikuwa Sh. 15,000 hadi Sh. 18,000.

Wilayani Kahama lita tano inauzwa Sh. 20,000 awali ilikuwa ikiuzwa Sh.17,500.

Mkoani Morogoro, robo lita kwa sasa inauzwa Sh.1,000 kutoka Sh.750 ya mafuta ya alizeti, dumu la lita tano linauzwa Sh.22,000 awali ilikuwa Sh.18,000, wakati dumu la lita tatu lililokuwa likiuzwa Sh.12,000 linauzwa Sh. 15,000.

Mkoani Mbeya awali bei ya jumla ilikuwa Sh. 11,000 kwa dumu la mafuta ghafi lita tatu linauzwa Sh. 13,000.

Mkoani Mwanza ndoo kubwa ya mafuta inauzwa Sh. 67,000 kutoka Sh. 59,000 bei ya awali.

HABARI KITAIFA

# TCRA yawatoa hofu watumiaji simu

**Na Mary Geofrey**

SIKU chache baada ya kuibuka sintofahamu kutokana na kampuni za simu kupandisha gharama za vifurushi, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema inaendelea na kazi ya kurudisha mfumo wa awali.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema mabadiliko ya kurudisha vifurushi vya awali bado yanaendelea kufanyiwa kazi.

"Kurudisha mabando (vifurushi) kama ilivyokuwa awali ni 'process' (mchakato), hivyo suala hilo tunaliangalia upya na ni kazi inayoendelea kwa sasa," alisema Dk. Bakari.

Alisema kampuni za simu zinaendelea kutoa huduma za vifurushi vipya kwa sababu vimewekwa kwenye mfumo ambao hauwezi kubadilishwa kwa haraka.

"TCRA tunafuatilia suala la bando kwa ukaribu kwa watoa huduma kuhakikisha vifurushi vyote vinarudi katika mfumo wa awali kama ilivyokuwa hivi karibuni," alisisitiza.

Wakati huo huo, TCRA imeondoa zuio kwa watoa huduma za simu kuendeleza kuwatumia watu binafsi bila kuathiri usajili sahihi wa laini za simu kwa alama za vidole wakati wakiendelea kufanya tathmini upya ya namna bora inayoweza kutumiwa na watoa huduma.

TCRA inawataka watoa huduma binafsi kuhakikisha wanatumia weledi katika kufanya kazi yao ya usajili wa laini za simu.

Februari 16, mwaka huu, baada ya kuwa na kikao na watoa huduma za mawasiliano ya simu, TCRA iliwaelekeza kusitisha kuwatumia watu binafsi katika usajili wa laini za simu kwa alama za vidole ifikapo Mei Mosi, mwaka huu.

Badala yake, ilitaka usajili ufanyike katika maduka au sehemu maalum kwa mujibu wa kanuni za usajili wa laini za simu za mwaka jana.

# Vita ya urais TLS leo, serikali yaonya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKATI macho na masikio ya Watanzania yakiwa mkoani Arusha ambako leo magwiji wa sheria nchini, watamchagua Rais atakayekiongoza Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), serikali imewasihi kuepuka kujiingiza kwenye masuala ya kisiasa na uanaharakati.

Badala yake, imewataka viongozi wao kuzingatia misingi na jukumu lao la kisheria la uanzishwaji wa chama hicho.

Akizungumza jana, wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa TLS, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Sheria na Katiba, Dk. Amon Mpanju alisema:

"Niwaombe uongozi uliopo, wanachama na uongozi ujao tushirikiane na serikali kwa sababu wote tunajenga nyumba moja, kama kuna matatizo karibuni tukae meza moja tuzungumze, ila tuepuke kujiingiza kwenye masuala ya siasa na uanaharakati.

"Haya ndio malengo au misingi ya uanzishwaji wa chama hiki, kwa misingi hiyo ukitazama sheria ya chama chetu, kifungu cha 4, imeanisha malengo ya kuanzishwa kwa chama chetu na lazima tujielekeze huko kama chama cha kitaaluma na lazima tuyaishi kwa viongozi waliopo na watakaochanguliwa."

Wagombea watano wanaotifuana kumtafuta Rais wa TLS ni Wakili Flaviana Charles ambaye ni Mkurugenzi wa Kituo cha Bussness & Human Rights Tanzania, na aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Dk. Edward Hosea.

Wengine ni Wakili Albert Msando, Rais wa zamani wa TLS, Francis Stolla na Wakili Shehzada Ujalli.

Kwa mujibu wa Mpanju, chama hicho chenye wanachama takribani 10,000 kilipoanzishwa mwaka 1954 kikiwa na wanachama tisa, kiliweka malengo yake matano, ikiwamo kukuza maadili ndani ya elimu ya taaluma ya sheria nchini na kusaidia serikali na mahakama katika masuala yote ya sheria.

Aliyataja malengo mengine ni pamoja na kuwezesha upatikanaji na kuendeleza elimu ya sheria nchini, pamoja na kusaidia masuala yote yanayohusu sheria na utawala wa sheria pamoja na huduma ya uwakili, kuwakilisha kulinda na kukuza maslahi ya wanachama ndani ya tasnia ya sheria na kukuza na kulinda maslahi na masuala yote wa wanachama.

Aidha, Mpanju alisema kila mmoja ni vyema akafahamu kuwa uanzishwaji wa vyama mbalimbali tangu wakati wa ukoloni, ulikuwa wa malengo mahususi ikiwamo kuunganisha nguvu na kutetea maslahi ya wanachama kwenye tasnia hiyo.

Alisema serikali inachokifanya ni kuweka mifumo na miundombinu ya kuwezesha vyama, hivyo kukua na kuendelea kwa kuchukua hatua mahususi, ikiwamo kuweka sheria, kuongeza udahili kwa watu wanaosomea sheria, kuongeza vyuo vinavyotoa taaluma ya sheria na kutoa wakufunzi ili tasnia hiyo ikue na kuleta tija.

Pamoja na mambo mengine, alisema wapo baadhi ya wanachama ambao ni mawakili, mienendo yao sio mizuri kutokana na kuchukua mashauri ya watu na kutowakilisha mahakamani na kwenye vyombo vya utoaji haki japo wamechukua na fedha zao.

Vile vile, alikemea tabia ya baadhi yao wanaotoa kauli za kashfa kwa baadhi ya majaji na mahakimu kuacha kufanya hivyo, kwani wanajeruhi na kuharibu uhusiano baina ya chama na mihimili ya serikali.

Aliongeza serikali haitaruhusu mawakili wa serikali kufanya shughuli zao hizo kama mawakili binafsi, kwani itasababisha mgongano wa maslahi na matokeo yake kutumia baadhi ya vifaa vya serikali kwenye matumizi binafsi.

Awali, Rais wa TLS anayemaliza muda wake, Dk. Rugemeleza Nshala, alisema katika kipindi cha uongozi wake amekutana na changamoto nyingi ikiwamo za kutishwa kufanya kazi hasa kwenye kesi za utakatishaji fedha na baadhi ya wanachama wao kukutana na kesi za kutaka kufutiwa uwakili na baadhi wakijikuta wakifutiwa uwakili.

"Lakini hatuwezi kupiga kelele kwa kila kitu, katika hili tunaendelea kupambana kwa kufungua kesi katika ngazi za mahakama zinazofuata, kwa sababu huo mwanya upo na tunaamini tutafanikiwa na naomba viongozi wajao wahakikishe wanasimamia haki za wanachama na kuzingatia utii wa sheria," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

## TAARIFA KWA UMMA

**KUONGEZWA KWA MUDA WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WANUFAIKA WA MWISHO (BENEFICIAL OWNERS)**
**Dar es Salaam, Aprili 08, 2021**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) unapenda kuwataarifu Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kwamba Waziri wa Viwanda na Biashara, kupitia Tangazo la Serikali Na. 189 la tarehe 12 Februari 2021 ameongeza muda wa miezi kumi na miwili (12) kuanzia tarehe 1 Januari, 2021 kwa ajili kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) kwa kampuni zilizosajiliwa kabla ya tarehe 1 Julai, 2020.

Takwa hili la kuwasilisha taarifa tajwa ni matokeo ya marekebisho ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 (Finance Act, 2020) kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners).

Aidha Kifungu cha 459A cha marekebisho hayo, ambacho kilizitaka Kampuni zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 kabla ya tarehe 1 Julai, 2020 kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) ndani ya kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Julai, 2020.

BRELA kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Kanuni za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) zitakazoweka bayana utaratibu wa kukusanya na kuhifadhi taarifa hizi.

BRELA inawataka Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kutumia vizuri muda huu wa nyongeza kuwasilisha taarifa husika mapema na sio kusubiri muda wa mwisho ili kuepusha usumbufu wa namna yeyote unaoweza kujitokeza.

**Imetolewa na**
**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**

Jengo la Ushirka, Mtaa wa Lumumba, S.L.P. 9393, Dar Es Salaam, Simu: +255-22-2181344, 2180113, 2180141, 2212800, Nukushi: +255-22-2180371, barua pepe: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz , Tovuti: www.brela.go.tz

WaterAid

**EXPRESSION OF INTEREST FOR UNDERTAKING CONSULTANCY SERVICES FOR WaterAid COUNTRY PROGRAM EVALUATION**

WaterAid is an International Non-Governmental Organization with a vision of ensuring Safe Water Sanitation and Hygiene (WASH) for Everyone, Everywhere by 2030. WaterAid has had its operations in Tanzania since 1983 under the name "WaterAid Tanzania," which is registered as a Non-Governmental Organization in The Republic of Tanzania. WaterAid in Tanzania operates as a Country Programme and functional office of WaterAid UK; within the East African Region. The head office is in Dar es Salaam, Rufiji Street, Plot No.1469, Masaki Area within Kinondoni District.

**Background**
WaterAid Tanzania Country Strategy covers the period from April 2016 to April 2021.
This evaluation considers the period of 2016 to 2021 on the following Strategic Objectives (SOs):

**SO 1:** Influencing for greater accountability
**SO 2:** Mainstreaming WASH for effective partnerships
**SO 3:** Building capacity for strengthened WASH delivery systems
**SO 4:** Knowledge brokering for evidence-based decision making
**SO 5:** Innovation to solve problems and promote sustainability

**Purpose**

**The purpose of the Country Programme evaluation is to:**
- Assess the contextual relevance of the current Country Strategy against the backdrop of changes in the external environment.
- Assess the effectiveness against the Country's Strategic Objectives.
- Assess the added value and synergy of WaterAid's programmes with regard to the WASH sector in Tanzania.
- Capture the lessons learned from the implementation of the Country Strategy and reflect on the implications for the development of the following Country Strategy

**The role of a consultant is to:**
- Use the evaluation questions defined by the Country Programme as a starting point, refine the evaluation questions in consultation with the CP;
- Build on the guidelines, develop a detailed methodology for evaluating the Country Strategy. The exact methodology will include the supporting tools such as the analytical framework for document review, topic guides for conducting Key Informant Interviews, etc.;
- Submit an inception report, to be revised based on WaterAid's feedback;
- Analyse and synthesize internal documentation;
- Identify and analyse relevant external documents;
- Interview with WaterAid staff, government officials, INGOs, UN agencies, partners and CSOs
- Preparation of preliminary findings.
- Facilitation of reflection and validation workshop.
- Compilation of the final report using the template provided by WaterAid.

**WaterAid is looking for a consultant who meets the following requirements:**
- Experience in conducting evaluations of strategic plans and large, multi -faceted programs.
- Strong analytical skills in qualitative information.
- Knowledge of the WASH sector in the country (but not necessarily a WASH expert).
- Experience in policy analysis; Experience in conducting interviews with different types of Key Informants, including government officials, Ministry of Water (MoW), Rural Water Supply and Sanitation Agency (RUWASA), Ministry of Education Science and Technology (MoEST) and Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children (MoHCDGEC), INGOs, NGOs, and CSOs.
- Experience in facilitating participatory workshops.
- Good writing, presentation and communication skills.

**Timeframe**
It is anticipated that the consultancy will take between 15 and 20 days. Please submit a budget separating consultancy fees and reimbursable expenses. The budget should be inclusive of all required taxes stipulated by Tanzania Revenue Authority (TRA).

**Expression of Interest**
If you are interested in this consultancy, please submit your Expression of Interest to **NduhuraInnocent@wateraid.org** and CC **NicombolweKidagho@wateraid.org ZuenaMasumay@wateraid.org .**
Please visit **https://www.wateraid.org/tz/work-with-us** for an extended version of the advert.

Following a review of the Expressions of Interest submitted, shortlisted candidates will be invited for a short interview during the week commencing 26.4.2021, from which a final candidate will be selected.

**Please make sure your expression of interest includes the following:**
- **Short cover letter** explaining your motivation, relevant expertise and experience (max 2 pages).
- **The proposed approach**, building on the methodology proposed in the TOR. This should also explore how the consultant will mitigate the risk of COVID19 (max 1 page).
- Three examples of your written work with Country Strategy evaluation.
- **Budget**, with the distinction between your consultancy fees and reimbursable expenses.
- Curriculum Vitae.
- The contact details for **three referees.**



# Hivi ndivyo wananchi wanavyoibiwa gesi

**Na Romana Mallya**

HIVI ndivyo wananchi wanaotumia gesi katika matumizi ya nyumbani wanavyoibiwa kutokana na kuuziwa mitungi yenye ujazo pungufu.

Hali hiyo imebainika baada ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kufanya ukaguzi na kubaini wafanyabiashara wakubwa wa gesi kupunguza nishati hiyo kwenye mitungi midogo ya kilo 15 ili kupata faida.

Hivi karibuni, wananchi maeneo mbalimbali walilalamikia kuhusu mitungi ya gesi kwisha kwa muda mfupi huku maeneo mengi wauzaji wakifanya biashara hiyo bila kuwa na mzani kwa mujibu wa kanuni za EWURA.

Baada ya malalamiko hayo, Nipashe ilipita maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam na kubaini kuwa mnunuzi wa nishati hiyo ni vigumu kubaini kama ameuziwa gesi yenye ujazo unaolingana na mtungi kutokana na wauzaji kutokuwa na mizani.

Kutokana na kubaini kasoro hiyo, gazeti hili ilimtafuta Meneja wa Uhusiano na Mawasiliano wa EWURA, Titus Kaguo, ambaye alibainisha kwamba kanuni inasema mtu yeyote anayeuza gesi lazima awe na mzani na asipokuwa nao adhabu ni faini ya Sh. milioni tatu.

Pia alisema kanuni inawataka wauzaji wauze mitungi ya gesi ikiwa imefungwa na bila kuichanganya na kwamba endapo mtu ananunua mtungi, anachotakiwa ni kupima na vipimo vikionyesha ni sawa na kiwango kilichoandikwa kwenye mtungi maana yake gesi iliyomo ni halali.

Kagua pia alisema leseni ya EWURA kwa wauzaji wakubwa, inawataka wauze bidhaa ya kampuni moja na kwamba mamlaka iliwafuatilia mwaka huu kupitia kampeni yao na kukuta mitungi ikiwa chini ya kiwango cha ujazo wa gesi kilichotakiwa kuwamo ndani.

"Mitungi inayotumika kupunguzia zaidi ni ile ambayo imeandikwa kilo 66 ambayo ndani yake ina gesi kilo 38. Tulichokifanya tumewaambia wauzaji wakubwa kwamba moja, wasiuze gesi holela, mitungi hiyo mikubwa iuzwe kwenye taasisi," alisema.

Kaguo alifafanua kuwa mtungi wa gesi wa kilo 38 ukichukua bei yake kimsingi inakuwa rahisi kuliko mtungi wa gesi wa kilo 30.

"Hivyo ni rahisi mtu mwenye mtungi wa gesi wa kilo 38 akapunguza gesi yake kwenye mtungi wa gesi wa kilo 15 hata mitatu kwa kuweka gesi pungufu ya kilo 12 badala ya gesi kilo 15," alisema.

Alisema mitungi midogo hutumika kupunguzia na ndiyo kampeni ambayo EWURA wanapambana nayo.

"Tulikuwa tunafanya kampeni zetu kimya kimya lakini tumeamua kutoka kwa umma ili wajue. Tunawakamata wanalipa faini tunaachana nao," alisema.

Hata hivyo, alitaja changamoto iliyopo ni nishati hiyo kuuzwa kwenye maduka yanayochanganya na bidhaa zingine wakati inatakiwa ziuzwe yenyewe lakini kwa kuwa ni biashara ambayo ndiyo imeanza kupamba moto, EWURA haijaingia sana ili kuiacha ikue.

"Sasa imeshakua ndiyo maana unakuta tunatoa elimu. Watu wauze gesi kwa kufuata kanuni zinavyosema. Wawe na mzani, mitungi iwe imefungwa na isichanganywe.

"Tanzania zipo kampuni kama saba zinazojaza gesi na mpaka sasa EWURA tumezitembelea kampuni nne ambazo ni Taifa Gas, Lake Gas, Oryx na Manjis ili kujihakikishia miundombinu yao inafanyaje kazi," alisema.

Kuhusu maduka yenye bidhaa zingine ambayo yanauza gesi, Kaguo alisema kimsingi wanatakiwa kuwa na mizani.

"Tunachokifanya ni kwamba kwenye biashara ya gesi tofauti na nyingine, kuna mikataba ambayo inaingiwa, muuzaji mkubwa anaingia mkataba na mfanyabiashara mwakilishi wa kampuni ambaye naye anaingia mkataba na msambazaji ambaye anauza mitungi madukani," alisema.

Alisema EWURA inapokuta kosa kwenye duka la mtu hufuatilia mtungi ni wa kampuni gani na ndipo wanapomtoza faini ili aweze kumdhibiti wa chini yake.

"Kwa mfano tukikuta mtungi umepunguzwa gesi, tunaangalia kampuni husika, tunawaangalia hawa wakubwa, huku chini tunawaacha wao wafuatilie," alisema.

Meneja huyo alisema elimu wanayoitoa hivi sasa ina lengo la kuwajulisha wafanyabiashara wa gesi kuwa EWURA inakuja kwa ajili kufuatilia suala hilo.

# Mwanafunzi auawa kwa kupigwa radi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MWANAFUNZI wa kidato cha nne Shule ya Sekondari Kabugaro, Wilaya ya Bukoba, mkoani Kagera, Gisela Osward (18), amefariki dunia kwa kupigwa na radi huku mwalimu Charles Alphonce akijeruhiwa.

Akithibitisha kifo cha mwanafunzi huyo, Mganga Mfawidhi wa Hospital ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, Museleta Nyakiloto, alisema majira ya 5:00 asubuhi alipokea maiti na majeruhi waliotokana na kupigwa kwa radi

"Walivyopokelewa na wataalamu walianza kufanya vipimo ndipo walibaini mwanafunzi ameshakufa kutoka na mwili wake wote kuunguzwa na radi na mwalimu wake kujeruhiwa sehemu za miguuni na anaendelea na matibabu," alisema Nyakiloto.

Akizungumzia radi ilivyosababisha kifo cha mwanafunzi huyo, mwalimu Alphonce alisema, majira ya saa 3:00 asubuhi akitokea darasani baada ya kumaliza kipindi aliambatana na mwanafunzi huyo kuelekea ofisini.

Alisema, wakiwa njiani karibu na ofisi aliona mwanga unawazunguka na kuanguka chini, walimu na wanafunzi wengine walifika eneo waliokuwa wamelala.

"Ilikuwa imebaki umbali kidogo kufika ofisi nilikuwa na mwanafunzi tunatembea kwenda huko, ghafla mwanga ukapiga mbele yetu na kuanguka chini nikishindwa kutembea sikuwa nasikia chochote miguuni nilipooza nikageuka kuangalia nyuma alipokuwa mwanafunzi yeye alilala palepale," alisema Alphonce.

Alisema wanafunzi na walimu walifika na kutubeba kuongozwa ndani ya gari na kutufikisha hapa hospitali bahati mbaya mwanafunzi alikuwa ameshafariki na mimi nipo naendelea na matibabu.

Mmoja wa ndugu wa marehemu Adinani Said, alisema, alipokea taarifa kutoka shuleni kuwa mwanafunzi huyo amepigwa radi na amepelekwa hospitali ya rufani ndipo alipofika shuleni hapo na kupewa maelezo ya kwenda hospitali walipofika walipokea taarifa za kifo cha ndugu yao.



Baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Mtongani, Kata ya Kunduchi, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, wakiangalia sehemu ya fremu zao za biashara 13, zilizovunjwa usiku wa kuamkia juzi, katika eneo la Skanska. Katibu wa kikundi cha wajasiriamali wadogo wa Mji Mpya, Shaaban Kwenyula, alidai kuwa zoezi la uvunjaji lililongozwa na Diwani wa kata hiyo, bila ya wao kujua sababu za kuvunjiwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwenyekiti kortini kwa tuhuma za kujipatia mil. 15/- kwa udanganyifu

**Na Mwandishi Wetu,** KYELA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, Godfrey Katule, amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kyela akituhumiwa kujipatia Sh. milioni 15 kwa njia ya udanganyifu.

Katule ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Ikimba, alifikishwa mahakamani hapo jana mbele ya Hakimu wa Wilaya, Paul Barnaba na kusomewa shtaka la kujipatia kiasi hicho cha fedha ambazo ni za Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kita.

Mwenyekiti huyo kabla ya kufikishwa mahakamani aliwekwa ndani katika Kituo cha Polisi Kyela mjini na baadaye kufunguliwa kesi hiyo ambayo mtuhumiwa mwingine katika kesi hiyo ni Furaha Burton.

Hata hivyo, baada ya kusomewa shtaka hilo watuhumiwa hao walikana kutenda kosa hilo na wapo nje kwa dhamana na kesi hiyo imeahirishwa hadi Aprili 27, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana nje ya mahakama baada ya kuachiwa kwa dhamana, mwenyekiti huyo wa halmashauri alisema alikamatwa juzi na polisi wapatao sita baada ya kutoka kwenye semina ya vikundi ambavyo halmashauri imeandaa Sh. milioni 110 kwa ajili ya kuvikopesha.

"Wakati tunatoka kwenye semina ghafla nikakuta nje kuna gari la polisi likiwa na askari sita na bunduki, wakaniambia niingie kwenye gari lao, lakini nikawaambia wanieleze sababu za kukamatwa kwangu, wakanieleza natuhumiwa kujipatia fedha Sh. milioni 15 kwa njia ya udanganyifu ambazo zilitoka kwa DC (Mkuu wa Wilaya)," alisema.

Katule aliwaomba askari hao aingie kwenye gari yake ya halmashauri aongozane nao kwenye kituo cha polisi, lakini walikataa kwa madai wamekuwa wakimwita mara kadhaa afike kituoni lakini anakaidi kufanya hivyo.

"Baadaye nilikwenda polisi nikawekwa ndani baada ya kutoa maelezo ambayo nilikana kutenda kosa hilo na baadaye nikapewa dhamana, na tutarudi tena mahakamani Aprili 27, 2021," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya Kyela, Kitta, alisema taarifa za kukamatwa na polisi Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, alizipata baada ya kupigiwa simu kutokea Dodoma na Mbunge wa Kyela, Ally Mlagila.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

**YAH: TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA BODI YA USHAURI YA WAKALA WA ELIMU NA MAFUNZO YA UVUVI (FETA)**

Kufuatia uteuzi wa **Dkt. Blandina Robert Lugendo** kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA). Waziri wa Mifugo na Uvuvi, **Mheshimiwa, Mashimba Mashauri Ndaki,** kwa mamlaka aliyonayo chini ya Sheria ya Wakala za Serikali (The Executive Agencies Act) ya mwaka 1997 Sura ya 245 ikisomwa pamoja na marejeo yake ya mwaka 2009, na Amri ya Rais ya Kuanzisha Wakala wa Serikali (Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi) ya mwaka 2011, Tangazo la Serikali Na. 356/2011, amewateua wafuatao kuwa Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA);

1. Profesa Zackaria Samwel Masanyiwa;
2. Dkt Modesta Medard Ntara;
3. Bibi Prisca Jovin Ngonyani; na,
4. Dkt. Robert Jeremiah Kayanda.

Uteuzi huu ni wa miaka mitatu kuanzia tarehe 29 Machi, 2021. Katibu Mkuu na Menejimenti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Sekta ya Uvuvi inawapongeza Mwenyekiti na Wajumbe kwa Uteuzi huu.

Dkt Rashid A.Tamatamah
**KATIBU MKUU - UVUVI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila laheri TLS, itendeeni haki nafasi ya urais

**LEO** Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), kinafanya uchaguzi wa rais ambaye kwa mujibu wa katiba yao anakaa madarakani kwa muda wa mwaka mmoja.

Licha ya uchaguzi wa nafasi nyingine, lakini macho ya wengi yapo kwenye nafasi ya rais, ambayo ina wagombea watano, baadhi wametumia vyema mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kueleza kwanini wanagombea nafasi hiyo kubwa katika chambo hicho.

Sheria iliyoanzisha TLS imeeleza malengo tisa ambayo ni kudumisha na kuboresha viwango vya mwenendo wa taaluma ya sheria nchini, kusaidia upatikanaji walimu ya sheria kwa wanasheria.

Mengine ni kusaidia serikali na mahakama kwenye mambo yanayohusu sheria na utungaji wake, na hii ndio inaifanya TLS mdau mkubwa wa kutoa maoni kuhusu maboresho au utungaji wa sheria.

Aidha, lengo jingine ni kuwawakilisha na kuwalinda mawakili na watu wa kwenye taaluma ya sheria kwenye utekelezaji wa sheria nchini.

Pia, inasaidia jamii kwa kuipa elimu na msaada wa kisheria pale inapohitaji.

Yapo mengi ya msingi ambayo TLS ina wajibu wa kuyasimamia ipasavyo na kuwa kiungo muhimu baina yake na serikali, mawakili na jamii, ili kufikia malengo ya haki kwa wanajamii wote.

Matarajio ya jamii ni kuwa wanachama wa TLS wataleta mgombea sahihi ambaye ataendana na mazingira sahihi ya shughuli za sheria na mawakili nchini.

Wanachama wa TLS ndio wanajua kati ya wagombea wote nani atafaa na atakuwa mgombea sahihi kwa sifa za kitaaluma, uzoefu na uelewa mkubwa wa masuala ya sheria, mifumo na jamii ambayo ni mnufaika.

Tunatambua kuwa TLS kwa kushirikiana na mahakama inatoa msaada wa kisheria kwa wananchi ambao hawana uwezo wa kuajiri wakala katika mahakama ambazo ni lazima mshtakiwa au mlalamikaji awakilishwe na wakili.

Wapo mamia ya wananchi wanakosa msaada wa sheria kiasi cha haki za msingi kupotea, na ni muhimu sana huduma hii ikapanuliwa ili kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa haraka zaidi.

Ni muhimu kuwafikia wananchi wenye uhitaji wa huduma hiyo hasa maeneo ya vijijini ambayo miundombinu yake bado ni changamoto, na mwananchi anasafiri umbali mrefu kufuata huduma hizo.

Wapo waliofungwa siyo kwa sababu walistahili, lakini kwa kuwa walikosa huduma ya uwakili au msaada wa sheria tangu mwanzo wa shauri lake.

Tunatambua kazi inayofanyika ikiwamo kuwatembelea wafungwa katika Magereza mbalimbali na kutoa msaada wa kisheria kwao, lakini bado kuna uhitaji mkubwa kulingana na mashauri yaliyopo au ukandamizaji haki unaojitokeza.

Pia, tunarajia wataleta mgombea ambaye atasisitiza umuhimu wa kuifikia jamii kutoa elimu ya uelewa wa masuala mbalimbali ya sheria, ili wasiingie kwenye tatizo ni kwa kutoelewa sheria.


Tunawatakia uchaguzi mwema TLS na ni matarajio ya jamii watachagua kiongozi sahihi kwa wakati sahihi, kwa kuhakikisha anayepatikana ataifikisha katika malengo yake ikiwamo ubunifu wa kuifikia jamii.

Mawakili wana changamoto zao na wanapochagua kiongozi wanatarajia alete mabadiliko makubwa, ili sehemu kubwa ya changamoto zitatuliwe, ikiwamo kuisaidia jamii kwa kiasi kikubwa.

Tunajua haki ya kila mtu imetajwa katika katiba ya nchi, na mchakato wa kutoa haki unahusisha vyombo vingi, lakini kwa msaada wa wakili haki stahiki ya mtu itapatikana kwa wakati katika muhimili wa utoaji haki.

Kilio cha kuminywa kwa haki ni kikubwa na hasa katika mihimili ambayo ni lazima wanasheria hususan mawakili wanatakiwa kuwatetea wananchi, na ndiyo umuhimu wake katika kutekeleza malengo yake ya msingi unaoonekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# Tuzingatie alichosema Waziri Lukuvi, kupafanya ufukwe Coco 'mali adimu'

**KILA** eneo la ardhi duniani, nchi kavu au bahari, lina thamani yake.

Ufukwe ni kati ya rasilimali za kipekee ambazo hunufaisha wakazi wa eneo husika, iwapo kutakuwapo na ubunifu fursa za kibiashara. Tanzania tuna bahati hiyo kwa kuwa tuna bahari ya Hindi.

Zipo nchi na hata mikoa kadhaa ambayo haina bahari na kutegemea kuja katika maeneo yenye bahari kwa ajili ya kutembea, kupumzika na familia.

Dar es Salaam ni moja ya mikoa iliyo na ufukwe wa bahari ingawa mikoa yote iliyopo ukanda wa Pwani, hapa nchini kuna fukwe.

Coco Beach, ufukwe maarufu wa bahari ya Hindi, eneo la Oysterbay wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, ambako umaarufu wake awali ulitokana na watu kupatumia kwa ajili ya kupumzika, huku wajasiriamali wa vyakula, nao si haba wanajiingizia kipato.

Eneo hilo lilipata umaarufu wa kuwa na mihogo ya kukaangwa iliyoandaliwa na wafanyabiashara waliokuwapo eneo hilo, kabla hapo awali kuondolewa kupisha ujenzi.

Kwa kurejea Unguja, mfumo unaotumika katika eneo la Forodhani, ungeigwa hata ufukwe wa Coco, ingekuwa na hadhi ya mafanikio.

Darasa la Forodhani, Unguja ni kwamba kuna bustani zenye shughuli nyingi, hasa baada ya jua kuchwa, kando ya bahari ya Hindi.

Achilia mbali wenyeji kutembelea eneo hilo, hata watalii vilevile hukusanyika kwenye bustani hiyo iliyobuniwa kama soko, ikitoa fursa ya biashara

Hapo panauzwa mihogo, viazi, dagaa, samaki, pweza, chapati sambusa na vingine vingi, biashara inayowaingizia kipato wakazi wa eneo hilo wakiwa na mtaji mdogo.

> **Mnamo Februari mwaka huu, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi, alifanya ziara katika ufukwe wa Coco, akitoa maagizo ya kuvunjwa eneo ambalo ujenzi wake alisemai ni uvamizi na akataka eneo hilo kuachwa wazi, patumike kwa ajili ya wananchi kupumzika na wafanyabiashara.**

Mnamo Julai mwaka 2009, asasi ya kimataifa ya Khan Trust for Culture (AKTC), ilipafanyia marekebisho eneo la Forodhani kwa gharama ya Dola za Marekani milioni, tatu sawa na takriban Sh. Bilioni saba, ikipanua wigo wa kibiashara na kupendezesha mandhari.

Bustani hiyo ambayo ni ya kale, bado imeendelea kunufaisha wakazi wa eneo hili, pia inaweza kufanyika kwenye maeneo yaliyo na fukwe kama za Dar es Salaam.

Mnamo Februari mwaka huu, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi, alifanya ziara katika ufukwe wa Coco, akitoa maagizo ya kuvunjwa eneo ambalo ujenzi wake alisemai ni uvamizi na akataka eneo hilo kuachwa wazi, patumike kwa ajili ya wananchi kupumzika na wafanyabiashara.

Akiwa mahali hapo, ameshauri kuboreshwa eneo hilo kwa ajili ya mapumziko na si ilivyokuwa awali kwamba ujengwe uwanja.

Fukwe za bahari zikiboreshwa madhari yake na mamlaka husika bila ya kutumia gharama kubwa, kwa kuweka maeneo ya watu kupumzika yanaweza kuwa chanzo cha mapato kwa halmashauri husika pamoja na kuwaingizia kipato wananchi.

Hiyo ina maana itatoa fursa kwa vijana ambao ni kundi kubwa nchini, wengi wao wakiwa hawana ajira, pamoja na wanawake waliojikita kwenye shughuli za uzalishaji hivi sasa.

Kundi hilo ambalo wengi wao wamo mijini kutafuta ajira, wakipata fursa na maeneo sahihi ya kibiashara watajiajiri.




Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kukabidhi zawadi ya Sh. Milioni 1.9 kwa Wakala wa Tigo, Paison Baruti (kushoto), aliyeibuka mshindi wa promosheni ya Waka Push. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajawazito walalamikia kutozwa 10,000/- vipimo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAJAWAZITO katika Kata ya Ngaya, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wamelalamika kutozwa Sh. 10,000 kila mmoja ikiwa ni gharama ya vipimo wanapofika katika kituo cha afya Ngaya kuanza kiliniki zao.

Walisema kuwa kipimo cha wingi wa damu wanatozwa Sh. 3,000, cha magonjwa ya zinaa Sh. 5,000 na cha mkojo Sh. 2,000 isipokuwa kipimo cha maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ndicho kinatolewa bure.

Getruda Dickson, mkazi wa Kijiji cha Mwashimbayi, alitoa malalamiko hayo jana mbele ya diwani wa kata hiyo, Kisusi Ilindilo, aliyefika katika kituo cha afya hicho, kusikiliza na kutatua kero za wagonjwa baada ya kupigiwa simu kuwa wajawazito wanatozwa Sh. 10,000 ndipo wapate vipimo.

Alisema kuwa, wajawazito wanaofika katika kituo cha afya Ngaya kuanza kliniki wanalazimika kutoa kiasi hicho cha fedha ndipo wapate huduma za vipimo na kwa mwanamke ambaye hana fedha hizo anakosa matibabu na kulazimika kwenda nyumbani bila kuhudumiwa au kuanza kiliniki.

"Vifo vya kinamama wajawazito na watoto kamwe havitakwisha kama wataendelea kutozwa fedha wanapofika kiliniki, wapo wanaokata tamaa na kuamua kwenda nyumbani na ikitokea tatizo wanatibiwa kienyeji badala ya kituoni," alisema Dickson.

Naye Nindwa Marco, mkazi wa Bulige alisema, lugha chafu zinazotolewa na wahudumu zinasababisha wagonjwa wengi kutopatiwa huduma stahiki kutokana na hofu ya kujieleza matatizo waliyonayo kwa muuguzi au daktari.

Kwa upande wake, diwani wa kata hiyo, Ilindilo alisema, katika vikao vya baraza la madiwani na kamati ya afya, elimu na maji hawajawahi kupitisha kiasi hicho, kinachotozwa na wahudumu, anachojua huduma kwa wajawazito, watoto wadogo chini ya miaka mitano na wazee wenye misamaha ni bure. Alisema iwapo hali hiyo itaendelea katika kituo hicho malalamiko hayo atayafikisha kwa mwajiri wao

# Mawaziri wakutana kupitia kanuni, sheria TV- mtandao

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, wamekubaliana kupitia upya kanuni, sheria na miongozo mbalimbali kuhusu televisheni mtandao kwa kuangazia katika vipengele vya usajili, kanuni, sheria, miongozo pamoja na tozo ikiwa ni pamoja na kuweka mifumo rafiki ya usajili na malipo kwa kuangalia uwezekano wa kupunguza tozo na kufanya uchambuzi yakinifu wa nani anatakiwa kulipia kwa kuendana na matumizi husika.

Aidha, mawaziri hao wameazimia kuwa kuna haja ya kuangaliwa upya muundo mzima wa uwajibikaji wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa wizara zote mbili pasipo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya mamlaka hiyo katika sekta ya mawasiliano na utangazaji nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari na Kitengo cha Mawasiliano cha Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, mawaziri hao walikutana pamoja na mambo mengine, kujadili namna ya kutekeleza maelekezo waliyopewa na Rais Samia Suluhu Hassan, Aprili 6, mwaka huu, alipokuwa akiwaapisha makatibu wakuu, manaibu katibu wakuu na wakuu wa taasisi mbalimbali kuhusu kufanya marekebisho ya kanuni na sheria zinazosimamia vyombo vya habari nchini hususani televisheni mtandao.

Maelekezo mengine ambayo Rais Samia aliyatoa kwa TCRA Aprili 6, mwaka huu ni pamoja na kuongeza utoaji wa elimu kwa umma kuhusu usajili, kanuni, sheria na taratibu zote za televisheni hizo mtandao kwa kuhakikisha zinawekwa kwa uwazi kwa wananchi kwa kuambatana na elimu ya matumizi sahihi ya mtandao kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji wa pamoja.

Pia, mawaziri hao walipitia hoja mbalimbali zinazotakiwa kufanyiwa mapitio na maboresho ikiwa ni pamoja na chaneli za runinga zinazotakiwa kuonekana katika visimbuzi bila malipo (FTA), kanuni za maudhui na utoaji wa adhabu kwa vituo hivyo vya redio na runinga kwa kuwekewa ukomo kwa mujibu wa kanuni na kutaka adhabu ziwe zenye lengo la kulea na si vinginevyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa, mawaziri hao kwa pamoja wamejipanga kuhakikisha sekta wanazozisimamia hususani katika maeneo ambayo yana mwingiliano katika utendaji wao, yanafanyiwa maboresho ili kuendana na hali halisi ya sasa ya kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na kufanyia kazi malalamiko ya wananchi wao.

**The Following USED Machine are available for immediate sales.**

1. **Motor Grader**




2. **Soil Stabilizer Machine**



Managing Director
Estim Construction Co. Ltd
P.O. Box 19716

For Further Enquiry, please contact.
0784261345, 0746941956

**TAARIFA KWA UMMA**



**BW. MICHAEL ANATE MURO**

KAMPUNI YA BEKA TRADING COMPANY LTD YA DAR ES SALAAM INAPENDA KUUTANGAZIA UMA WA WATANZANIA KUWA **BW. MICHAEL ANATE MURO** MWENYE PICHA HAPO JUU SIO MFANYAKAZI WA KAMPUNI YETU TANGU MWEZI WA 11 MWAKA JANA, NA HIVYO KAMPUNI HAITAHUSIKA NA CHOCHOTE ATAKACHOKIFANYA, AIDHA KAMPUNI IMETOA TAARIFA KWENYE KITUO CHA POLISI

## TANGAZO

MuCoBa

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31/12/20
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 12/31/20 | Mwaka Uliopita 12/31/19 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 620 | 485 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 64 | 223 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 4,030 | 1,558 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 13,961 | 10,985 |
| 12 | Mali nyingine | 3,597 | 3,334 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 621 | 440 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **22,893** | **17,025** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 15,101 | 14,493 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 95 | 95 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 580 | 475 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 634 | 243 |
| 28 | Madeni | 2,786 | 3,045 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **19,199** | **18,354** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **3,694** | **(1,329)** |
| | | - | - |
| | | - | - |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,887 | 2,763 |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | - | - |
| 32 | Akiba ya Mtaji | (5,996) | (4,526) |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 716 | 410 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 87 | 24 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | | |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **3,694** | **(1,329)** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1,843 | 1,450 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 815 | 2,382 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 16.14% | -7.81% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 13.20% | 11.10% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 92.45% | 75.80% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.98% | 64.52% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 85.00% | 82.43% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 4.20% | 12.92% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 34.47% | 5.43% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWAKA UNAOISHIA 31-12-2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 12/31/20 | Mwaka Uliopita 12/31/19 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,836 | 3,304 |
| 2 | Gharama za Riba | (959) | (667) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 2,877 | **2,637** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (188) | (99) |
| | | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | 779 | 937 |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 779 | **937** |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | (2,652) | **(2,888)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,366) | (1,376) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (132) | (165) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,154) | (1,347) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | 816 | 587 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 100 | (177) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | 716 | 410 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | | |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | 716 | **410** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 59 | 60 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 22 | 26 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 1 |
| | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 4.09% | 2.50% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 60.55% | -43.97% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 61.54% | 68.17% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 20.52% | 20.26% |

Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho
kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31/12/2020

| | | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Mwaka wa sasa** | | | | |
| | **Salio la mwanzo wa mwaka** | **2,763** | **(4,116)** | **24** | **(1,329)** |
| | Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 716 | - | **716** |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | **-** |
| | Miamala na Wanahisa | 6,124 | - | - | **6,124** |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | **-** |
| | Ziada ya Kisheria | - | - | - | **-** |
| | Tengo la Ziada ya Jumla | - | (1,817) | - | **(1,817)** |
| | Mengineyo | - | (63) | 63 | **-** |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,887** | **(5,280)** | **87** | **3,694** |
| | | | | | |
| | **Mwaka Uliopita 2019** | | | | |
| | Salio la mwanzo wa mwaka | **2,662** | **(5,619)** | **2,363** | **(594)** |
| | Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 410 | - | **410** |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | **-** |
| | Miamala na wanahisa | 101 | - | - | **101** |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | **-** |
| | Ziada ya Kisheria | - | - | - | **-** |
| | Tengo la ziada ya Jumla | - | 1,030 | (1,858) | **(828)** |
| | Mengineyo | - | 63 | (481) | **(418)** |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **2,763** | **(4,116)** | **24** | **(1,329)** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA WA MWAKA UNAOISHIA 31-12-2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 12/31/20 | Mwaka Uliopita 12/31/19 |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 817 | 587 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | Hasara Katika Mali | 414 | 353 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (984) | 77 |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | | |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 608 | 1,668 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | | |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | 437 | 549 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (989) | (1,096) |
| | Kodi Iliyolipwa | (38) | (31) |
| | Mengineyo (Bainisha) | (448) | (216) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli** | **(183)** | 1,891 |
| | **Zauendeshaji** | - | - |
| | | | - |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana** | - | - |
| | **na Shughuli za Uwekezaji:** | - | |
| | Gawio lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | (92) | (30) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa** | - | - |
| | **(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(92)** | **(30)** |
| | | | - |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (200) | (312) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | 5,000 | 101 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (2,077) | (1,307) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | **2,723** | **(1,518)** |
| | **Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | | |
| | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | - |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | 2,448 | 343 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo M | 2,266 | 1,923 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo M | **4,714** | **2,266** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAOISHIA 31/12/2020

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina Na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Philipo Raymond<br>Meneja Mkuu | ……………………………...….. (Imesainiwa) | 27/Mar/2021 |
| Kelvin Mushi<br>Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | …...……………..…………….. (Imesainiwa) | 27/Mar/2021 |
| Hilda Valerian<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | ……………………………….......... (Imesainiwa) | 27/Mar/2021 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| Jina | Tarehe |
|---|---|
| 1. Prof.Domicus Kasilo………………………… (Imesainiwa)<br>Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi | 27/Mar/2021 |
| 2. Bw.Kitova Mungai ……………………………..... (Imesainiwa)<br>Mwenyekiti | 27/Mar/2021 |

### MUCOBA BANK PLC- CHARGES AND FEES- 2020

| SAVINGS ACCOUNT | CHARGES AND FEES |
|---|---|
| **Individual Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Joint Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Juvenile's/ Minor Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Biashara Savings Account** | |
| Account Opening minimum amount | 65,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 50,000 |
| Monthly Service Fee | 5,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Saccos Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 55,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 100,000 |
| Monthly Service Fee | 2,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Elimu Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 10,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Malengo Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | See Table below |

**Malengo account interest rates are as follows:**

| Period | | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | | 4% |
| 6 months | | 5% |
| 12months | | 6% |

**FIXED DEPOSIT ACCOUNTS**

| Period | Range | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 4.00% |
| 6 months | Up toTzs 9,999,999.00 | 4.50% |
| 9 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 5.00% |
| 12 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 6.00% |
| 24 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 7.00% |
| 36 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 8.00% |

FDR of Tzs **10,000,000** and above is **negotiable** at management discretion.

**GENERAL CHARGES AND FEES**

| GENERAL CHARGES/ FEES | TZS |
|---|---|
| | |
| **Dishonored/Unpaid cheque** | |
| Fund related | NA |
| Technical | NA |
| | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS** | |
| Cash deposit at branch | Free |
| Cheque clearing (up to Tzs 1,500,000) | 15,000 |
| Cheque clearing (above Tzs 1,500,000) | 1% |
| Cash withdrawal- (less Tzs 5,000,000) | 1,000 |
| Cash withdrawal- (Tzs 5,000,000 and above) | Tzs 1,000 plus 0.08% of excess above 5,000,000, Max |
| | Tzs 150,000 |
| Account closure | 15,000 |
| Dormant account reactivation | 3,000 |
| Dormant account monthly Fee | 1,000 |
| Premature/cancelled Fixed Deposit Fee | No interest given |
| Interim Statement Fee | 1,000 |
| Audit confirmation Fee | 10,000 |
| Balance certificate Fee | 20,000 |
| Reference Letter | NA |
| TT Outward local-TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| TT Inward local- TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| Salary Processing (per entry) | 2,500 |
| Bank Guarantees | NA |
| Balancy Inquiry | 100 |
| Money Transfer | 12,000 |
| ATM card replacement | 15,000 |
| ATM w/drawal Fee (on us) | 1,300 |
| To other bank ATMs w/drawal Fee | 1,300 |
| ATM mini statement | |
| Wallet to Bank | 1,000 |
| SMS alart | 1,000 |
| Bank to Wallet (Below Tzs 100,000) | 1,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 100,000-199,999) | 1,300 |
| Bank to Wallet (Tzs 200,000-299,999) | 1,700 |
| Bank to Wallet (Tzs 300,000-399,999) | 2,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 400,000-499,999) | 2,500 |
| Bank to Wallet (Tzs 500,000-599,999) | 3,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 600,000-699,999) | 3,500 |
| Savings account interest rates | 2% |

## Watakiwa kujiwekea akiba tangu utotoni

**Na Beatrice Moses**

Benki ya NMB imesisitiza wananchi kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba tangu utotoni ili waweze kutumia fedha wanazopata vizuri.

Meneja wa Kanda ya Magharibi, Sospeter Magese, akizungumza katika hafla fupi ya utoaji zawadi kwa washindi wa promosheni ya Bonge la Mpango ambapo mshindi kutoka Nzega alikabidhiwa pikipiki ya miguu mitatu maalum kwa kubebea mizigo.

Alisema mbali ya kujenga utamaduni huo kupitia bahati nasibu wanayoiendesha pia wanataka kurudisha sehemu ya fedha kwa wananchi na wateja wao.

"Sisi tuna malengo makubwa mawili ikiwemo la kujenga utamaduni wa kuweka akiba na kurudisha sehemu ya fedha kwa wateja na wananchi," alisema. Akizungumza baada ya kukabidhiwa zawadi ya pikipiki ya miguu mitatu aliyoshinda, mkazi wa Nzega, Habiba Bushiri, alisema biashara yake ya keki ndiyo inayompa kipato chake na hatimaye kujishindia bahati nasibu.

"Tunapaswa kuweka jitihada zote katika biashara tunazofanya pasipo kujali ni ya aina gani na ina ukubwa au mtaji kiasi gani," alisema.

Habiba alieleza kwamba alianza kuweka akiba miaka mingi,akijijengea utamaduni wa kuweka akiba pale anapofanya biashara yake na hata ilipoanza bahati nasibu ya NMB,hakuwa na tatizo kujiwekea akiba kwa manufaa yake na famllia yake.

Magese,alieleza kwamba bahati nasibu ya benki hiyo,ilianza Februari mwanzoni, inalenga kujenga tabia ya wananchi kujiwekea akiba pamoja na kurudisha kiasi cha fedha kwa wananchi.

Wakati huo huo, watu kumi walishinda bahati nasibu droo ya tano iliyoendesha tawi la NMB Mihayo,wawili pikipiki ya miguu mitatu aina ya LIFAN na mmoja gari dogo la mizigo yaani Kilikuu,wakitoka maeneo tofauti hapa nchini na kushuhudiwa na mwakilishi wa bodi ya michezo ya kubahatisha nchini.

Katika bahati nasibu hiyo,baadhi ya wateja walikosa zawadi kwa kushindwa kupatikana au simu zao kuita pasipo kupokelewa na kwa mujibu wa mchezo huo,wanakosa sifa ya kupata zawadi zao.




Wafanyakazi wa kiwanda cha kutengeneza magari mapya nchini cha Tanzania GF-Vehicle Assembly Ltd, wakiangalia gari ikishushwa kwenye reli za kutengenezea magari ikiwa ni gari la 100, kutengenezwa kwenye kiwanda hicho, kwa kipindi cha miezi minne, katika sherehe iliyofanyika Kibaha, mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kituo cha mafuta kuuzwa kushindwa kulipa kodi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

BARAZA la Ardhi na Nyumba, Wilaya ya Morogoro limetoa uamuzi wa kukifungia, kukamatwa na kuuzwa kwa kituo cha mafuta na gesi cha Kampuni ya Lake Oil kilichopo katika kiwanja namba moja Block E, eneo la Msamvu, Manispaa ya Morogoro kwa madai ya mmiliki wake kushindwa kulipa kodi ya ardhi aliyokuwa anadaiwa kwa hiyari.

Baraza hilo limetoa amri hiyo kupitia kwa Kampuni ya Udalali ya Mwamba Millenium Company Limited na kwamba baada ya kukifunga, kukamata na kuuza mali hizo, kampuni hiyo ya udalali inapaswa kupeleka mauzo hayo katika Baraza hilo kwaajili ya kukabidhiwa kwa mshinda tuzo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungwa kwa kituo hicho, Ofisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Huruma Valency, alisema mmliki wa mali hiyo, Sajaad A Rasool, anadaiwa kodi ya ardhi ya serikali jumla ya Sh. 26,850,250. Alisema kabla ya kulifikisha shauri hilo kwenye Baraza hilo walishawasiliana na mmliki huyo mara kadhaa akikumbushwa kulipa kodi hiyo, lakini amekuwa akikahidi na hivyo kuliomba Baraza hilo kutoa amri ya kuuza mali hizo.

Naye Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Morogoro, Frank Minzikutwe, alisema wamepewa majukumu ya kukusanya kodi ya ardhi kwa mkoa mzima jumla ya Sh. bilioni 11.3 na kwa Manispaa pekee wanapaswa kukusanya Sh. bilioni 4.4 na wameamua kuwapeleka mahakamani wote wanaodaiwa kodi ya ardhi.

Alisema kuwa mdaiwa huyo kwa kipindi kirefu amekuwa akikahidi kulipa kodi hiyo licha ya kumtaka kufika ofisini ili kuweka utaratibu wa jinsi ya kulipa deni hilo, lakini amekuwa hafiki na wala hatoi taarifa zozote.

Aliwatangazia wakazi wa Mkoa wa Morogoro kuwa operesheni hiyo itafanywa mkoa mzima na wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi watafikishwa mahakamani ili mali zao ziuzwe ili kulipa deni hilo.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Udalali ya Mwamba Millenium Company Limited, Nathan Kaunda, alisema wameamua kukifunga kituo hicho kwaajili ya kutekeleza amri halali ya Baraza hilo la Ardhi na Nyumba kupitia kesi namba 86/2020 iliyotolewa uamuzi tarehe 10/03/2021, iliamrisha kukamatwa na kuuzwa kwa mali zilizopo kwenye kiwanja kilichopo.

Meneja wa Kampuni hiyo ya Lake Oil, aliyejitambulisha kwa jina moja la Mgingi, alipotakiwa kutoa maelezo alidai yeye sio msemaji wa kampuni hiyo na hana mamlaka ya kutoa taarifa zozote.

# Lipumba: Corona imeongeza umaskini

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimesema mlipuko wa virusi vya corona umesababisha idadi kubwa ya wananchi kuishi kwenye wimbi la umaskini.

Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Prof. Ibrahim Lipumba, alisema hayo jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maazimio ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa yaliyotolewa kupitia kikao cha siku mbili kilichofanyika kuanzia Aprili 10.

Alisema wananchi, hasa walioko mjini, wanaishi kwenye wimbi la umaskini hali iliyochochewa zaidi na mlipuko wa corona.

"Benki ya Dunia (WB) inakadiria kwa kutumia kigezo cha umaskini cha taifa, idadi ya Watanzania maskini imeongezeka kutoka asilimia 26.1 mwaka 2019 hadi asilimia 27.2 mwaka 2020. Watu 600,000 wameingia katika dimbwi la umaskini mwaka 2020," alisema.

Lipumba alisema zaidi ya Watanzania milioni 15 ni maskini kwa kutumia kigezo cha umaskini cha taifa.

"Baraza kuu linahuzunishwa na ukosefu wa furaha kwa Watanzania. Taarifa ya furaha duniani ya mwaka 2021 inaonyesha Tanzania ni ya 94 kati ya nchi 95 zilizofanyiwa utafiti wa furaha ya wananchi wao," alisema

Prof. Lipumba alisema baraza kuu linaishauri serikali kuasisi mapinduzi ya kilimo ili kufanikisha maendeleo ya viwanda ambayo yanategemea ukuaji wa sekta ya kilimo inayozalisha chakula cha wafanyakazi na malighafi za viwandani.

Pia alisema baraza kuu linaiomba serikali kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

"Serikali itafute vyanzo vipya vya mapato na kuhamasisha ulipaji wa kodi, iboreshe utendaji na ufanisi wa mamlaka za rufaa za kodi ili kusaidia usikilizaji na umalizaji wa kesi, iongeze idadi ya wataalam wanaoshughulikia mapingamizi ya kodi," alisema.

Kuhusu viongozi waliohama chama hicho na kwenda vyama vingine, Prof. Lipumba alisema baraza limeacha milango wazi kwa wanachama waliohama warejee ili kukijenga na kusisitiza kuwa CUF itashiriki uchaguzi wowote kwa kutegemea hali ya kisiasa.

Pia imeitaka serikali ipitia makubaliano ya mikataba 17 iliyoingiwa kati ya Tanzania na China wakati wa awamu ya nne za kuitekeleza yenye faida na nchi.

Kuhusu mradi wa bandari ya Bagamoyo, alisema baraza hilo linaishauri serikali kufanya upembuzi yakinifu na taarifa zake ziwekwe wazi ili vipengele vyenye matatizo viondolewe.

# Ataka kushuka bei za vifurushi

MBUNGE wa Kilolo (CCM), Justin Nyamoga, ameitaka serikali kushusha bei ya vifurushi ili Watanzania wamudu kutumia mitandao katika shughuli zao za kibiashara.

Nyamoga akiuliza swali, alisema wananchi wanategemea kutumia vifurushi vya bei ndogo, lakini ongezeko la bei linawakatisha tamaa.

Alihoji lini serikali itarudia mpango wake wa kushusha bei ya vifurushi ili Watanzania wakiwamo wa-Kilolo ambao wanataka kutumia vifurushi hivyo katika shughuli zao za kibiashara watumie vifurushi nafuu.

Akijibu, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Andrea Kundo, alisema serikali inaangalia suala hilo.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji lini serikali itajenga minara ya simu katika Kata za Masisiwe, Nyanzwa, Irole na Ibumu ambazo zina shida kubwa ya mawasiliano.

Akijibu, Naibu Waziri Kundo, alisema jimbo la Kilolo lina kata 24 ambapo Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imeishakamilisha utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata tatu ambazo ni Lugalo (Halotel), Udekwa (Vodacom) na Ukwega (Tigo na Halotel).

"Pamoja na jitihada hizi za Serikali baadhi ya kata za jimbo hili zinachangamoto za upatikanaji wa huduma za mawasiliano kama vile Kata za Masisiwe, Nyanzwa, Ibumu na baadhi ya maeneo ya Kata ya Irole. Jiografia ya jimbo hili ya milima na miti mirefu inaathiri ukubwa wa eneo la upatikanaji wa huduma za mawasiliano kutokea mnara uliposimikwa," alisema.

Aidha, alisema katika Kata ya Irole kuna baadhi ya maeneo yanapata huduma za mawasiliano kupitia mnara wa mawasiliano wa HTT uliobeba watoa huduma watatu ambao ni Airtel (2G), Vodacom (2G na 3G) na Tigo (2G na 3G).

"Pamoja na uwepo wa huduma za mawasiliano kutoka kwa watoa huduma niliotaja, bado kuna maeneo ya Kata ya Irole yana changamoto za upatikanaji wa huduma za mawasiliano,"alisema.

Alibainisha serikali kupitia mfuko huo iliifanyia tathmini Kata ya Ibumu na hatimaye kukijumuisha Kijiji cha Ilambo katika zabuni ya Awamu Tano ya Mradi wa kufikisha mawasiliano mipakani na kanda maalum.

"Mradi huu unatekelezwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL Corporation) ambapo mikataba ya utekelezaji wa mradi huo ilitiwa saini tarehe 6, Julai 2020,"alisema.

Hata hivyo, alisema mradi huo utakapokamilika utahudumia vijiji vya Ibumu, Kilala Kidewa, Ilambo na Kilumbwa.

"Serikali kupitia UCSAF itavifanyia tathmini vijiji vya Kata za Masisiwe, Nyanzwa na baadhi ya vijiji vya Kata ya Irole ambavyo havipati huduma za mawasiliano kupitia kwa watoa huduma wanaotumia mnara wa HTT uliopo.

# Wilaya kame kipaumbele ujenzi, ukarabati mabwawa

SERIKALI imesema inaendelea na mpango wa ujenzi na ukarabati wa mabwawa kwa kila wilaya husussan ambazo ni kame.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zainab Katimba. Katika swali lake, Mbunge huyo alisema ki-jiographia Tanzania ipo kwenye ukanda wenye mvua za kutosha.

"Je, Serikali imejizatiti vipi kuhamasisha zoezi la uvunaji wa maji ya mvua kwa matumizi ya wananchi?" alihoji.

Akijibu, Naibu Waziri Mahundi, alikiri kuwa nchi ipo kwenye ukanda wenye mvua za kutosha, hivyo ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua ni muhimu kwa kuwa itawezesha kuwa na maji ya uhakika kwa kipindi chote cha mwaka bila kujali hali ya hewa.

Vilevile, alisema miundombinu hiyo ni muhimu kwa kuwa itawezesha kudhibiti mafuriko na hivyo kuokoa miundombinu, ikiwemo ya huduma za maji pamoja na mali na maisha ya wananchi. "Katika kutimiza azma hiyo, mkakati mwingine ni Wizara ya Maji kukutana na TAMISEMI kwa lengo la kuhusisha mashule kujenga gata za maji na matanki, pia kuhamasisha wananchi wanapojenga nyumba zao waweke miundombinu rafiki ya kukusanya maji," alisema. Hata hivyo, alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21, Wizara imekamilisha ukarabati wa bwawa la Mwadila lililopo Wilaya ya Maswa Mkoa wa Simiyu, usanifu kwa ajili ya kukarabati mabwawa matatu ya Itobo liliopo Wilaya ya Nzega.

Pia alisema Engukument lililopo Wilaya ya Monduli na Horohoro lililopo Wilaya ya Mkinga na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa mawili ya Muko na Chiwanda yaliyopo Wilaya ya Momba.

"Usanifu wa Malambo ya kunyweshwea mifugo (Charcodams) sita umekamilika katika mwambao wa barabara kuu ya Dodoma-Babati ikihusiha Wilaya za Bahi malambo mawili na Chemba malambo manne," alisema.

Aidha, alisema serikali inaendelea na mpango wa kujenga mabwawa ya kimkakati ya Kidunda (Mto Ruvu) Farkwa (Mto Bubu) na dembera au Lugoda (mto Ndembera).



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, akijibu baadhi ya maswali yaliyoulizwa bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ujenzi vituo vya afya kuendelea

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, amesema serikali itaendelea kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya, vikiwamo vilivyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi kulingana na upatikanaji wa fedha.

Dk. Dugange alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Lushoto (CCM), Shaaban Shekilindi, ambaye alisema jimbo lake lina kituo kimoja cha afya, na sasa wananchi wameanza kujenga vituo viwili vya Gare na Ngwelo.

"Je, Serikali ipo tayari sasa kutoa fedha kwa ajili ya kumalizia vituo hivyo, na itafanya hivyo lini?" alihoji.

Akijibu, Dugange alisema ili kuboresha huduma za afya katika Wilaya ya Lushoto Serikali kuanzia mwaka wa fedha 2017/18-2019/20 imetoa Sh.bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wodi ya wazazi katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto pamoja na ukarabati na upanuzi wa Vituo vya Afya vya Mlola, Kangagai na Mnazi ili kuviwezesha kutoa huduma za dharura za upasuaji.

"Machi 2021, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto Sh. milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma matatu ya zahanati, "alisema.




**Na Augusta Njoji,** DODOMA


Ukurasa 12

Vijue 'vigezo na masharti' vya kamati za Bunge kabla haijamhoji mdaiwa

UCHUMI

# Soko la Machinga ghorofa maridadi, huduma yake imejaa 'madudu'

## • Viongozi wakubali, ufumbuzi kigugumizi kwa jiji jipya



Sehemu ya jengo la Soko la Machinga Complex. **PICHA: MTANDAO**

**Na Yasmine Protace**

JIJINI Dar es Salaam, kuna masoko mengi makubwa na madogo, pia yanatofautiana kwa ukubwa wa majengo na kiwango cha biashara mahali hapo.

Panapozunguziwa eneo maarufu la Soko la Machinga au Machinga Complex, ukubwa wake ni wa kipekee unajulikana sana jijini Dar es Salaam na pengine nje ya jiji. Hata hivyo, inapogeuzwa 'upande wa pili wa shilingi' kuna shida ya biashara kusuasua mno.

Umma wa jiji la Dar es Salaam, sasa unahoji kulikoni kuwapo majengo makubwa mahali, lakini matarajio ya ujenzi na hadi miaka iliyopita yana sura 'sifuri'?

Nipashe iliamua kuzuru hapo, ambako kimsingi kuna kivutio cha majengo hasa mtu anapokuwa katika barabara ya Uhuru kuliona majengo hayo yalivyokaa, eneo la Ilala, jirani kabisa na Kariakoo.

**WENYEJI WANENA**

Juma Hassan ni mfanyabiashara katika soko hilo, 'anayeripea' nguo za mitumba eneo la mwanzo wa soko, jirani na ngazi ya kupandisha ghorofa, pametawaliwa na harufu ya mikojo.

Anasema, ni mahali ambako vijana wahuni maarufu kwa jina 'mateja' wanashinda hata kulala, hivyo uhalisia wa mazingira ya mahali hapo inatoweka.

Hassan anataja lingine linalounga na adha hiyo, ni vyoo vibovu, hakuna maji na koki zake zimeharibika. Huduma ya maji zinatumika kupitia mapipa yanayojazwa na kuna wakati chooni kunabaki bila ya maji.

Mfanyabiashara wa vinwaji, Mwajuma Ally, analalamika: "Tunalipa ushuru, tunalipa malipo ya kuingia chooni, tunalipa sehemu ya biashara, lakini bado vyoo ni vichafu makoki mabovu na havina maji ya uhakika."

Pia, anasema licha soko hilo kuwa na walinzi wa mgambo, bado pamebaki kuwa 'kijiwe' cha 'Mateja'

Hatibu Twaha, mfanyabiashara wa viatu, anashauri kuwekwa katika majengo taa muda wote, ulinzi kusimamia usalama wa mahali hapo, ikiwamo ngazi sokoni hapo wanakoshinda 'Mateja.'

pia, Twaha kutoka jamii ya Wakamsai anaeleza mshangao wake, kila mfanyabiashara sokoni anatambulika, lakini inashangaza kila waingiapo chooni wanatozwa Sh. 200 au walau iwe tozo ya mara moja kwa mchuuzi.

Aida John, anayeshona nguo sokoni hapo, anasema kodi ya kila mwezi ni Sh. 20,000, na anaendelea: "Mtu ukikosa kulipa mwisho wa mwezi wanaokuja kulichomelea geti lako ili usiendelee na biashara na ulifanikiwa kulipa unatozwa faini Sh. 5000."

Mwingine ni Baraka Msham, anayesema kutokana na soko kukosa maji salama na ya uhakika, wapo wapangaji mama lishe, wanawaacha na kitendawili wakijiuliza maji ya kupikia wanayapata wapi.

Hivyo, anashauri haja ya wataalamu afya kufika sokoni kufuatilia wachuuzi wa chakula, mama lishe, wanakopata maji ya kupikia, kwani ana shaka nayo.

Aidha, Jamila Jamal mfanyabiashara anayechangia hoja kwamba, kila mwezi wanalipa Sh. 3000, wakati huo, wao wafanyabiashara ndio wanakubaliana na walinzi wakiwalipa Sh. 5,000 kila mwezi kwa ajili kuwakusanyia taka, ujumla wake wanajikuta kutozwa pesa nyingi.

"Wasitutoze kodi kubwa,hili jengo juu halina watu kabisa,inatakiwa tuangaliwe katika tozo zao, ili na sisi tuhamasishe watu waje kufanya kazi katika jengo hilo ambalo kuna nafasi haijajaa huko juu," anasema.

**MENEJA SOKO**

Meneja wa Soko hilo, Lecho Mkama, alipotakiwa na Nipashe kufafanua madai hayo, hakujibu chochote kutokana na Halmashauri ya Manispaa Ilala, kubadilishwa kuwa ndio Halmashauri ya Jiji la Dar es Salama hivi karibuni, hadi sasa haina mkurugenzi.

"Madai yako yatajibiwa pale Mkurugenzi (wa jiji Dar es Salaam) atakapokabidhiwa ofisi na akanipa kibali cha kuzungumza na wewe, nitayasema yote yanayohusu soko," anatamka Meneja wa Soko.

Pia, Nipashe ilipomtafuta Ofisa wa Afya wa Jiji Dar es Salaam, Reginald Mlay, akasema soko lilikuwa chini Jiji na wanaanza kupokea majengo na wataangalia suala la miundombinu na vitu vingine, kisha watajua maeneo yanayotakiwa kurekebishwa.

Anasema, wataanza na ukaguzi na upungufu utakaobainika utafanyiwa kazi, huku linalohusu usalama wa biashara mamalishe na uwapo wa huduma za maji, hakuwa tayari kufafanua akidai hajapatembelea hivi karibuni, japo anakiri haja ya kuwa na huduma nzuri za maji.

Mlay anakiri biashara kufanyika sokoni Machinga, na hivyo kuna umuhimu wa ukaguzi.

DARASA LA KUSIMAMIA BAJETI ...

# Vijue 'vigezo na masharti' vya kamati za Bunge kabla haijamhoji mdaiwa

## • spika Ndugai awanyooshea kidole wavujisha siri

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

HADI sasa Bunge la Tanzania lina kamati zaidi ya 10. Miongoni mwake, imo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na ya Hesabu za Mitaa (LAAC).

Kwa utaratibu, mabunge ya Jumuiya Madola, kamati hizo zinapaswa kuongozwa na wenyeviti ambao ni wabunge wanaotokana na vyama vya upinzani.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, kamati mbali na kuchambua Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zimekuwa zikiwaita maofisa kutoka mashirika na taasisi za serikali, kujibu hoja zinazobainika kuwa na ukakasi.

Ili kuhakikisha wajumbe wa kamati hizo wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi, Taasisi ya WAJIBU iliyo chini ya aliyewahi kuwa CAG nchini kati ya mwaka 2006 hadi 2014, Mkurugenzi Mtendaji, Ludovick Utouh, imeendesha mafunzo maalum kwa wajumbe wa kamati tatu za Bunge.

Pia, kamati nyingine iliyopata mafunzo hayo bungeni jijini Dodoma mwishoni mwa wiki iliyopita, ni inayohusika na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC).

> **"Maandalizi ya namna ya kuendesha mahojiano ni pamoja na mpangilio wa maswali yatakayoulizwa, mjumbe atakayeuliza swali mahususi, muda utakaotumika kufanya mahojiano na mambo yatakayoruhusiwa kwenye mahojiano**



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), walipofika kukagua na kupata taarifa ya ujenzi wa hospitali ya Mji wa Makambako. .
**PICHA: MTANDAO**

### MBINU ZA MEDANI

Meneja Fedha na Utawala wa WAJIBU, Jackson Mmary, akiwasilisha mada kuhusu Mbinu za Medani za anazoziita 'Kuendesha Mahojiano,' anazitaja sifa kadhaa za mwendesha mahojiano.

Hapo anataja orodha ya kuwa; mvumilivu, msikivu, aliye na uelewa mzuri wa anachokihoji, anayejiamini, anayeelewa mazingira ya mahojiano, aliye na hisia iliyo na mwelekeo, anayejua alama za ishara, mtulivu na mbunifu.

Anasema kabla ya mahojiano, wajumbe wa kamati hizo wanapaswa kuwa na taarifa za kina za mada husika na nyingine za ziada kuhusu maeneo yatayofanyiwa mahojiano na historia ya suala, mtu, au taasisi husika.

Mengine katika hilo, pia inajumuisha sheria zinazosimamia jambo linalohojiwa au zinazohitajika, kufanyika uamuzi sahihi wa jambo linalofanyiwa mahojiano na maswali yanayotakiwa kuulizwa.

"Mambo muhimu ya kuzingatia kuhusu nani ahojiwe ni mhusika wa jambo linalohojiwa, mtu mwenye taarifa zinazohusu jambo linalohojiwa, mamlaka ya mtu anayehojiwa juu ya jambo linalohojiwa, tabia za mtu anayehojiwa na sheria za nchi zinazomlinda mhojiwa.

"Ni muhimu pia kuzingatia mahali pa mahojiano pawe na nafasi ya kutosha kwa wajumbe wote wanaohudhuria mahojiano, penye utulivu na usiri.

"Maandalizi ya namna ya kuendesha mahojiano ni pamoja na mpangilio wa maswali yatakayoulizwa, mjumbe atakayeuliza swali mahususi, muda utakaotumika kufanya mahojiano na mambo yatakayoruhusiwa kwenye mahojiano," anasema.

Mmary anawapa angalizo wajumbe wa kamati, dhidi ya vipingamizi vya mahojiano. Hapo anataja sheria zinazomlinda mhojiwa na zile zinazohusu kinachohojiwa, na mhojiwa kukataa au kushindwa kujibu maswali.

Aidha, anataja mhojiwa kutoelewa maswali na taarifa za uongo au kukosekana taarifa zinazohusu kinachohojiwa, ikiendana na maandalizi duni ya ama mhojiwa au mwendesha mahojiano.

### UFISADI NA RUSHWA?

Ili kubaini dalili za kutowajibika, rushwa na ufisadi, ofisa huyo wa WAJIBU anasema wajumbe wa kamati tajwa wanapaswa kusoma tabia na alama na ishara za mwili za walengwa wanaohojiwa.

"Walengwa wanapoitwa kuhojiwa halafu hawaonekani, walengwa wanapoitwa kuhojiwa, wakiulizwa swali wanakaa kimya au wanalia tu, majibu yasiyoendana na taarifa ambazo tayari mlikwishazipata, ni dalili za kuwapo hali hiyo," anaeleza.

Mmary anawakumbusha wajumbe wa kamati hizo kuwa, baada ya mahojiano, ni lazima nakala ya kumbukumbu ya mahojiano itiwe saini na mhojiwa, pamoja na mwendesha mahojiano.



Mkurugenzi Mtendaji wa asasi ya WAJIBU na CAg mstaafu, Ludovick Utouh.

Pia, anataja ya kuepukwa wakati wa mazungumzo yanajumuiosha matendo ya kumtishia, kumpiga, kebehi, kejeli au lugha chafu, kuuliza maswali binafsi na yasiyohusu mada inayohojiwa, pia kuwapo hasira kwa sababu yoyote ile wakati wa mahojiano.

"Bunge ndicho chombo kikuu cha nchi kilichoidhinishwa kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri serikali na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," Mmary anahitimisha.

### WOSIA KWA WABUNGE

Yona Killagane, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya WAJIBU, anatumia fursa hiyo kuwasilisha mapendekezo mawili kwa Bunge, akiamini itaongeza uwajibikaji nchini, ikiwamo, Bunge kuitaka serikali kuanzisha utaratibu wa Ripoti ya Msajili wa Hazina, kuwasilishwa bungeni.

Katika hilo anashauri Msajili wa Hazina, awe anaandaa ripoti za taasisi zote anazozisimamia, zikaguliwe na CAG, kisha kuwasilishwa bungeni zifanyiwe kazi na kamati husika.

Katika pendekezo la pili, Killagane anaeleza haja ripoti ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iwasilishwe bungeni, ili kuwapa nafasi wananchi kupitia wawakilishi wao wanashiriki katika mapambano dhidi ya rushwa.

"Tunapendekeza iwafikie pia wananchi ili washiriki mapambano dhidi ya rushwa. Ripoti ya PCCB (TAKUKURU) iliyowasilishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan Machi 28, mwaka huu, iwasilishwe bungeni ili iwe wazi na ijadiliwe kuwapa fursa wananchi," anapendekeza Killagane.

Mwenyekiti huyo, pia anampongeza Spika wa Bunge Job Ndugai, kwa ufanisi wa eneo lake la kazi, ikiwamo namna Inavyoipa ushirikiano taasisi hiyo inayoongozwa na CAG wa zamani, Ludovick Utouh, hata kuialika bungeni kutoa mafunzo kwa wajumbe wa kamati hizo tatu.

### NENO LA SPIKA

Katoka neno lake Spika Ndugai anapofungua mafunzo hayo, anaunga mkono mafunzo kwamba ni muhimu kwa wajumbe wa kamati hizo nyeti, kwa kuwa yanawajengea uwezo wa kufanya kazi zao kwa weledi.

Spika Ndugai, anawakumbusha wajumbe wa kamati hizo kutunza siri na kutojihusisha na vitendo vya rushwa katika kutekeleza majukumu yao.

"Wajumbe wa kamati hizi tunawategemea sana katika utendaji wa shughuli zetu bungeni. Mafunzo haya ni muhimu sana kwetu maana yanatujengea uwezo wa kufuatilia na namna ya kufanya mahojiano na maofisa wa tunawaoita kwenye kamati hizi," anasema.

Pia, katika hilo anatoa angalizo la hitaji la umakini, kwa kuwaagiza viongozi wa kamati kuwasilisha kwa Kamati ya Uongozi ya Bunge, majina ya wajumbe wake wenye tabia ya kuvujisha siri za kamati, ili wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Anaeleza hatia kwamba, baada ya kupokea majina hayo, kamati hiyo ambayo yeye ni mjumbe, inachukua hatua stahiki dhidi ya mmdaiwa husika, ikiwa ni pamoja na kuondolewa kwenye kamati husika.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Grace Tendega, anapokea mafunzo, akitoa ahadi: "Tunakuahidi Mheshimiwa Spika, tulichokipata hapa tutakifanyia kazi kwenye utekelezaji wa majukumu yetu."



## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Bomba hili liwanufaishe wazawa




**Na Joseph Kulangwa**

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais Yoweri Museveni wa Uganda, siku tano zilizopita, mnamo Aprili 11, walishuhudia utiaji saini mikataba ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kati ya serikali na kampuni ya uwekezaji Total ya Ufaransa na CNOCC ya China.

Bomba hilo lenye urefu wa kilomita 1,443, kipande cha nchini lina kilomita 1,147, ikianzia eneo la Ziwa Albert, Uganda eneo la Kabaale wilayani Hoima na litaishia Chongoleani, Tanga, likipita mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara hadi Tanga.

Mradi huo ni wa ubia kati ya Kampuni ya Mafuta ya Uganda (UNOC) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na kampuni hizo mbili za Ufaransa na China.

Mikataba mitatu ilitiwa saini; mmoja ukiwa ni huo wa ubia, pia wa uenyeji ambao ni kati ya serikali ya Uganda na wawekezaji ambao ni Total na CNOCC na wa tatu, ni masuala ya kodi na usafirishaji, ambayo ni Uganda kutia saini na kampuni hizo.

Mradi huo utakaogharimu fedha Dola za Marekani bilioni 3.5, unatarajiwa kutengeneza ajira zipatazo 10,000 wakati wa ujenzi na usafirishaji wa mapipa bilioni 6.5 ya mafuta hayo.

Mbali ya nchi hizo mbili pamoja na Afrika Mashariki kunufaika na mradi huo, vilevile unaonyesha uhusiano wa kihistoria baina ya mataifa haya mawili na hasa kwa kurejea hotuba ya Rais Museveni, akizungumzia mchango wa Tanzania katika kuyafurusha majeshi dhalimu ya Nduli Iddi Amin, Uganda.



NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

Hata hivyo, manufaa mengine husus an kwa Uganda, ni kwamba kukamilika kwa bomba hilo, kutaisaidia pia Uganda kuharakisha mpango wake wa kununua gesi kutoka Tanzania.

Bila shaka huu ni mradi mkubwa na mzuri kwa eneo hili la Afrika Mashariki, pia utanufaisha wananchi wanaoishi maeneo litakamopita bomba hilo, hususan katika mikoa minane nchini.

Hili linatakiwa kusimamiwa vema na serikali ili kuepusha upendeleo unaoweza kuutumkwa na baadhi ya wasimamizi wa mradi huo kwa kuitana watu kutoka mikoa lisikopita kwenda kufanya kazi katika sehemu hizo.

Pia, kama ilivyobainika katika ukaguzi wa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwamba kuna baadhi ya miradi mikubwa na hususan ya kimkakati nchini, walipelekwa wageni wasio na vibali kufanya kazi, huku wazawa wakiwa hawana cha kufanya na hivyo kuathirika kiuchumi.

Kwa mujibu wa sheria, ni marufuku taasisi au kampuni kuingiza kutoka nje nguvukazi inayoweza kupatikana nchini, isipokuwa kwa utaalamu ambao ni adimu, lakini fursa hizi za makandarasi wa kigeni, zimekuwa zikitumiwa vibaya na kuathiri vibaya Watanzania.

Kwa kuwa CAG ameshahadharisha na wabunge bila shaka wameliona, hatua zitachukuliwa, ili yaliyojitokeza katika ujenzi wa miradi ya Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere na wa Reli ya Kisasa (SGR) hayajirudii.

Kufanya hivyo, kutawafanya Watanzania kuona umuhimu wa miradi hiyo kutoka hatua za ujenzi hadi ukamilikaji na kuanza uzalishaji, hali itakayowapa moyo wa kujivunia na hata kuilinda dhidi ya maadui wanaotaka kuihujumu.

Lakini la msingi, ni kuhakikisha kuwa miradi hiyo inapokamilika, inakuwa endelevu na isije kuwa kama ilivyotokea, kwa bomba la gesi la Mtwara ambalo lilipokewa kwa bashasha na wananchi wa maeneo linakopita, lakini baadaye likalala na katika mtazamo kana kwamba halipo.

BIASHARA

# Ulivyo ushindani bidhaa, bei umeme na sera ya viwanda



Wateja wa umeme wa LUKU, wakiwa katika foleni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Nimi Mweta**

MOJA ya mitazamo muhimu katika kuanzishwa mradi wa bwawa la Nyerere eneo la Stiegler's Gorge, ni kupatikana umeme wa bei nafuu na wa kutosha, lengo ni kuondoa kero ya nishati hiyo iwe ya uhakika.

Imeshafahamishwa kwamba, gharama kutoka vyanzo vya maji umeme wa maji ni rahisi zaidi kuliko vingine, mfano gesi.

Akitoa hotuba ya kuanza ujenzi wa mradi huo, hayati Dk. John Magufuli, aliainisha bei za umeme katika nchi tofauti ambako bei ya umeme nchini Marekani (na Ulaya) iko chini sana, chini ya senti mbili za Marekani kwa kilowatt moja, wakati nchini ni kati ya senti tisa na 11 za Marekani (Sh. 207 hadi Sh.253).

Ikumbukwe, hata Marekani haimudu ushindani kwa bidhaa nyingi tu na China, bila kuweka 'mipaka ya ushuru wa forodha' ili bidhaa za Marekani ziwezeshe kuuzwa nchini humo. Ni hatua aliyoichukua Rais aliyepita Donald Trump kwa kupandisha ushuru kwa kiwango kikubwa au inaitwa kibiashara 'kwa hasira.'

Hiyo ina maana kwamba, nchi patakapopatikana umeme kutoka vyanzo vya maji, kutapunguza bei. Ila kuna maswali mawili yanabaki; ni kwa kiwango gani vyanzo hivyo vinaweza kupunguza bei hiyo?

Pili, ni kwa kiwango gani bei inabidi ipungue ili viwanda vyetu viweze kupunguza gharama kiasi cha kumudu ushindani dhidi ya bidhaa kutoka nje?

Maswali hayo hayawezi kujibiwa katika ngazi ya sera, ila baadaye, mradi huo utakapokamilika halafu tuangalie TANESCO ina uwezo wa kupunguza bei ya umeme kwa kiwango gani.

Ila tu mtu anaweza kuangalia vipengele vinavyochangia kuongeza bei za bidhaa na kujiridhisha kama hatua hiyo peke yake (chanzo cha umeme, kupunguza bei) inakuwa jawabu stahiki.

**MWELEKEO UJAO**

Kuangalia bei ya umeme kama kianzio muhimu cha bei za bidhaa zinazozalishwa kutokana na umeme huo, ni sahihi na kwa maana hiyo Tanzania sasa walau inaweza kutazamia kujenga viwanda vinavyomudu ushindani katika maeneo kadhaa, umeme wa maji utakapofika.

Tayari kuna hatua ya baadhi ya maeneo ya viwanda na sekta ya huduma kwa jumla, kumeenea umeme wa gesi, pale hazina ya gesi asilia ilipoanza kutumika muongo uliopita.

Wakati umeme wa ziada unapopatikana kutoka vyanzo vya mafuta mazito (wengine huita machafu) ilikuwa ni matumizi muhimu ya ofisini na hata viwanda vilivyokwishaanza kazi, haviwezi kufunga, si kujenga au kupanua viwanda katika mazingira hayo. Kwa maana hiyo dira ya viwanda ni hakika.

Tatizo ni kwamba, kuna mipaka ya 'mchongo' huo katika maeneo ambayo siyo bidhaa za watu wengi, kwa mfano sekta ya nguo kwa jumla (yaani pamba) kwani katika eneo hilo ushindani ni mkubwa sana, siyo kutoka China tu ila kote duniani.

> **Wakati umeme wa ziada unapopatikana kutoka vyanzo vya mafuta mazito (wengine huita machafu) ilikuwa ni matumizi muhimu ya ofisini na hata viwanda vilivyoanza kazi, haviwezi kufunga, si kujenga au kupanua viwanda katika mazingira hayo. Kwa maana hiyo dira ya viwanda ni hakika.**

Kuna uwezekano wa kuwa na ugumu katika ama kunazisha au hata kuendesha viwanda vya pamba kuzalisha nguo za kutumiwa na sehemu kubwa ya watu, kulinganisha na mavazi ya mitumba.

Hadi sasa kuna upenyo mpana unaonekana katika maeneo ambako pamba inatumika kutengeneza bidhaa za kitanashati, zishindane na zinazotoka nje, tena kwa ufanisi. Hivyo kuna 'mchongo' wa viwanda maalum, na siyo vile vya msingi.

Ushindani wa kibiashara kati ya China na Marekani, ukiamgaliwa una tofauti zao katika maeneo kadhaa ambayo vyanzo vya umeme havitajwi sana kama sababu mojawapo ya msingi.

Kinachoonekana zaidi, ni bei ya nguvu kazi, kwa maana ya viwango tofauti vya mishahara kati ya nchi hizo mbili, eneo ambako Tanzania ina kiwango kiasi fulani cha ushindani.

Hapo ndio maana wawekezaji wanajitahidi kutafuta njia za kujikita nchini, kama soko kubwa tarajiwa katika siku za usoni, kwani idadi ya watu sasa inaelekea kwa haraka huenda mwelekeo wa milioni 60, kabla ya kufika mwaka 2025.

Ikiwa vipato vya watu vitakuwa na uwezekano wa kupanda, kutakuwapo soko kubwa la bidhaa, lakini ili vipato viongezeke, inabidi bei ziwe ndogo kwanza, vipato vilivyopo viwe na uwezo zaidi wa kununua bidhaa.

Kwa kanuni ya msingi ya kuwekeza katika kiwanda ni kuangalia soko, gharama za kuwekeza na bei ambayo mzalishaji mpya atauza bidhaa zake, anatakiwa alenge bei ya kilicho kidogo kuliko aliyeko sokoni.

Ndiyo aina ya mustakabali uliotumika kueneza matumizi ya 'simu janja' katika ngazi tofauti za jamii duniani, ambako suala la msingi hapo siyo kianzio cha malighafi na umeme, ila bei ya nguvukazi.

Maana kuu ni kuhamisha viwanda hivyo kutoka Mashariki ya Mbali na halafu Asia ya Kusini hadi kuletwa nchini. Suala hilo limekuwa likitajwa inawezekana katika jamii yenye wakazi milioni 60, wakatengeneza 'simu janja'.

Kuna eneo ambalo bado haliajangaliwa katika mchanganuo huo wa vianzio vya nishati na bei ya bidhaa, yaani mitaji na ulipaji mikopo au fungani (bonds) zinazowezesha mitaji hiyo kupatikana.

Njia nzuri zaidi ya uwekezaji katika viwanda ni kwa mzalishaji wa nje anayetaka soko la nchini, badala ya kuletea bidhaa zilizoko tayari sokoni (zile za soko la juu kidogo, au 'pamba kali') aamue kuzitengeneza nchini.

Akiwa analeta mashine zake, anapata eneo kwa kununua ardhi, kulipa fidia na hahitaji mkopo wowote, bali anatumia ziada ya vifaa alivyo navyo, ataweza kuuza kwa bei ndogo zaidi.

Ndiyo maana kuuza umeme kwa bei ndogo unapotokana na mikopo ya kibiashara ya nje siyo rahisi; deni linatangulia.



Kituo kimojawapo cha huduma ya umeme, mkoani Kilimanjaro



## Mafunzo usafi wa mwili yanufaisha maelfu ya vijana

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA 48,000 katika mikoa minne watanufaika na mafunzo ya usafi wa mwili na mazingira yanayotolewa na shirika lisilo la kiserikali la Raleigh Tanzania, kupitia mradi wa vijana na mabadiliko chanya.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dodoma na mratibu wa mradi huo, Augostino Dickson, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya vijana walio katika mradi huo kufanya usafi katika soko la Mavunde Chang'ombe jijini Dodoma.

Alisema mradi huo hivi sasa unatekelezwa katika mikoa ya Dar es saalam, Dodoma, Morogoro na Iringa.

Aidha, alisema kuwa mradi huo umelenga katika kubadilisha mitazamo ya vijana katika masuala ya usafi ambayo yamekuwa hayapewi kipaumbele hali inayosababisha uchafu kuzagaa katika maeneo mengi.

"Lengo ni kuelimisha vijana kubadili mitazamo yao katika suala la usafi wao binafasi pamoja na mazingira ili maeneo kuwa safi na kusaidia kuepukana na magonjwa ya mlipuko, lakini pia kuwasaidia kuzitambua fursa zilizopo katika sula la usafi ambapo hivi kuna maeneo wanafanya taka kuwa fursa," alisema Dickson

Pia, alisema kuwa kupitia mradi huo walifanya tafiti kuona ni jinsi gani wanaweza kuendesha mafunzo ya usafi kwa vijana ili kuwabadili mitazamo yao.

Alisema, kutokana na utafiti huo waliandaa kitabu chenye mada sita ambazo wanazitumia kufundisha masuala mbalimbali ya usafi kwa vijana.

"Vijana ndiyo kundi kubwa katika taifa hivyo tuliona kuwa kwa kuwatumia wao tutaweza kubadili mitazamo iliyopo katika jamii na kuleta mabadiliko chanya katika suala la usafi," alisema.

Vilevile, alisema kuwa hivi sasa wamekuwa na vijana ambao wanafundisha kupitia kitabu hicho na kila mmoja wao baada ya mafunzo hayo anapaswa kufundisha wengine 50.

"Pamoja na kutoa mafunzo haya, pia tumekuwa tukishiriki katika kufanya usafi maeneo mbalimbali na kutoa msaada wa vifaa vya kufanyia usafi na kuhifadhia taka katika maeneo mbalimbali kama ambavyo tumefanya leo katika soko hili na shule ya Sekondari ya Dodoma," alisema Dickson.

# Ummy ampa siku tatu DED Chamwino

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ametoa siku tatu kwa Halmashauri ya Chamwino kuhakikisha mapato yote yaliyoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) yanaingizwa benki.

Vilevile, ameapa kutomvumilia mkurugenzi yeyote wa Halmashauri ambaye hatatenga asilimia 40 ya makusanyo kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Waziri Ummy aliyatoa maagizo hayo jana alipofanya ziara katika Halmashauri ya Chamwino na kuzungumza na watumishi wa halmashauri hiyo.

Alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo kuhakikisha ndani ya siku tatu mapato yote yaliyoainishwa na CAG kuwa yalikusanywa na hayajaingizwa benki yawe yameingizwa ndani ya siku hizo.

Pia, Waziri ummy alisema hatamvumilia mkurugenzi wa halmashauri yoyote ambaye hata tenga asilimia 40 ya fedha anazozikusanya na kuzielekeza katika shughuli za maendeleo na kuzitaka halmashauri kuweka kipaumbele katika miradi ya afya katika maeneo yao.

Kadhalika, aliwaagiza watendaji wa Halmashauri nchini kuacha tabia ya kuwadharau na kupuuzia ushauri wa wanasiasa hususani madiwani wanapowashauri katika mambo mbalimbali ya kiutendaji katika maeneo yao.

Alibainisha kuna baadhi ya watendaji wanapuuzia na kudharau ushauri wa wanasiasa katika mambo mbalimbali hasa yanayohusu vyanzo vya mapato katika halmashauri hizo.

"Nitoe wito kwa Halmashauri zote hapa nchini kuacha mara moja hii tabia ya kuwadharau wanasiasa, kwa kudhani madiwani wote ni darasa la saba, hapana, sasa hivi kuna madiwani wana PhD (shahada ya uzamivu), na hata kama darasa la saba hao wamechaguliwa na wananchi na wanajua mambo mengi sana yanayohusu wananchi," alisema Waziri Ummy.

Alizisisitiza sekretarieti za mikoa kuhakikisha zinatimiza majukumu yao katika kuzishauri halmashauri hasa katika ukusanyaji na matumizi ya mapato katika serikali za mitaa na kujenga utamaduni wa kuzitembelea na kufanya tathmini katika yale waliyoyapanga.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema kwa kipindi kirefu halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imekuwa haifanyi vizuri licha ya juhudi nyingi ambazo wamezifanya katika kuhakikisha inaimarika katika kipengele cha kukusanya na katika matumizi sahihi ya mapato ya Serikali.




Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Eliaman Sedoyeka (kulia), akikabidhiwa mkataba na Mwakilishi wa Chuo cha Uhasibu cha Kimataifa chenye makao makuu yake nchini Uingereza (ACCA), Genald Lazaro, baada ya kutiliana saini makubaliano ya ushirikiano, jijini Dodoma jana. Anayeshuhudia (katikati) ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi, Hamadi Masauni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mawaziri, Balozi wa Marekani wajadiliana fursa za uwekezaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo na Wizara ya Uwekezaji Geoffrey Mwambe, wamekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, ili kujenga ushirikiano katika fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mazungumzo hayo, Prof. Mkumbo alisema mazungumzo yao wamelenga kukuza biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Marekani. "Leo tumekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Marekani, kuona namna ya kukuza ushirikiano wetu uliopo kati ya nchi hizi mbili, bado tuna fursa nyingi na kubwa za wafanyabiashara wetu kutumia fursa hiyo," alisema.

Alisema katika mazungumzo hayo wamekubaliana kuweka jitihada za kuhakikisha nchi hizo mbili zinazidi kushirikiana katika nyanja za kiuwekezaji na kuleta manufaa na kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara kukuza uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja.

Waziri huyo alisema pia wamezungumzia kuhusu mazao ya kimkakati hasa katika kuchakata badala ya kuuza malighafi, ili mazao hayo yachakatwe hapa nchini na kuuza bidhaa. Naye, Waziri Mwambe alisema wamezungumzia kuhusu uwekezaji katika sekta mbalimbali ikiwamo ya afya, na kuridhika na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika uwekezaji.

Alisema wawekezaji kutoka Marekani wameonyesha wapo tayari kuja kuwekeza nchini, na kwamba tayari kuna kampuni imeonyesha nia ya kuja kuwekeza katika sekta ya mawasiliano katika kampuni ya simu, na kampuni ya utalii kutoka Arusha imeonyesha nia ya kutaka kuongeza zaidi uwekezaji.

"Tumeongelea uchakataji wa mazao, na ukiangalia Marekani inanunua korosho nchi fulani, na ukiangalia sisi tunauza korosho ghafi na hizo nchi zinachakata na kuuza Marekani, na sisi sasa tunaweza kuzichakata nchini na kuuza Marekani," alisema Waziri Mwambe.

Alisema pia yapo mazao mengine ya kumkakati kama kahawa na pamba ambayo yatachakatwa na kuuzwa nje ya nchi hatimaye kama nchi kupata mapato kupitia kodi na kukuza ajira kwa wananchi ambao watapata ajira katika viwanda vitakavyoanzishwa.

Kwa upande wake, Balozi Wright alisema Tanzania na Marekani zimedumu katika ushirikiano kwa zaidi ya miaka 70 na kuahidi kuwa Serikali ya Marekani itashirikiana kwa dhati na kwa karibu na Rais Samia katika kuhakikisha wawekezaji kutoka nchi hiyo wanakuja kuwekeza nchini.

"Marekani imetengeneza historia kubwa katika kusaidia maendeleo ya Tanzania katika miradi ya kupambana na magonjwa, ulinzi, elimu, miundombinu na kwamba imechochea uhusiano kati ya Marekani na Tanzania kuimarika zaidi," alisema.



## DC ataka wazee kuwafunda vijana

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, amewaomba wazee wilayani hapa kuwafunda vijana ili waache majungu na uzushi badala yake wawafundishe uzalendo na kuchapa kazi.

Mfune alitoa rai hiyo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Wazee kilichokuwa na ajenda ya kufanya uchaguzi wa kumpata Mwenyekiti, Makamu, Katibu na Mweka hazina kwenye baraza hilo.

Alisema katika moja ya ziara alizowahi kuzifanya Hayati Dk. John Magufuli wilayani Mbarali, aliwaonya wananchi kuacha majungu na uzushi kwa madai kuwa vinachangia kudidimiza maendeleo na kuwakatisha tamaa wanaotamani kuwekeza.

"Naamini kupitia baraza hili mtatusaidia kuwafunda vijana ili kuachana uzushi pamoja na majungu kwa kuwa yanachochea visasi na chuki na kukwamisha shughuli za maendeleo," alisema.

Mfune aliwashauri wazee waliochaguliwa kuongoza baraza kuwa wawakilishi wazuri wa kusemea matatizo yanayowakabili wenzao zikiwamo huduma za matibabu.

Aidha aliwaomba wazee hao katika maeneo yao, kuendelea kushauri masuala mbalimbali kwenye jamii badala ya kukaa kimya na mambo kuharibika kwa ustawi wa wana Mbarali.

Akisoma risala mbele ya mkuu wa wilaya, Ofisa Ustawi wa Jamii, Winfrida Mahali, alisema mwaka 2012 halmashauri iliunda mabaraza ya wazee kwenye kata zote 20 lakini hayakuwa na nguvu hadi mwaka 2017 walipoyahuisha.

Mahali alisema mwaka 2003 Tanzania iliunda Sera ya Wazee ikiwa ni jitihada za serikali kuweka malengo na utaratibu mzuri kwa wazee ili kunufaika na rasilimali zinazopatikana nchini.

Mwenyekiti mpya wa Baraza hilo, Hezron Kapwela, kutoka Kata ya Chimala, aliahidi kushauri na kuishawishi serikali pamoja na wanasiasa kuboresha huduma kwa wazee wa wategemezi wao.

Alisema atahakikisha anaboresha mawasiliano kati ya wazee na serikali katika hali inayokubalika kikatiba kwa kuhakikisha huduma zinatolewa kwa usawa katika makundi yote.

# Tembo wavamia mashamba na kuharibu mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKAZI wa vijiji vitano vya Kata ya Igawa, Mbarali mkoani Mbeya, wako hatarini kukumbwa na baa la njaa baada ya zaidi ya tembo 100 kuvamia mashamba yao na kuharibu mazao.

Tembo hao wanadaiwa kutoroka katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuharibu mashamba ya mahindi, mpunga na viazi vitamu ambayo yanategemewa na wananchi hao kwa chakula na biashara.

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Gaitan Madindo, alisema tembo hao wameharibu zaidi ya ekari 400 za mazao hayo huku akidai kuwa hakuna madhara yaliyotokea kwa binadamu na makazi yao.

Alisema maofisa wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), walifika katika maeneo hayo kwa ajili ya kufanya tathmini ya uharibifu uliofanywa na wanyama hao pamoja na kuwaondoa ili kuokoa mazao.

Alisema tatizo lililotokea ni kiwango cha fidia ambacho wataalamu hao waliwaambia wananchi kuwa watalipwa kwa maelezo kuwa kiwango hicho kilizua mgogoro mwingine kutokana na kutoendana na uhalisia.

"Maofisa hao walisema serikali itawalipa fidia wananchi hao kila ekari moja Sh. 20,000 lakini wananchi hawajaridhishwa na kiwango hicho kwa sababu wanadai hakiendani na gharama walizotumia kwenye kilimo," alisema Madindo.

Diwani wa Kata hiyo, Nasoro Udes alimwomba Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega, kuwasaidiwa wananchi hao walipwe fidia haraka ili wanunue chakula kwa wakulima wa maeneo mengine ambayo hayajaathirika.

Alisema mara nyingi wakulima huwa wanapata shida na serikali kutakiwa kuwalipa fidia hazitolewi kwa muda mwafaka, hivyo kuwafanya wananchi waendelee kupata shida.

Mtega alifika juzi katika eneo hilo kwa ajili ya kuagalia uharibifu uliofanywa na wanyama hao pamoja na kuwapa pole wananchi. Alisema tatizo hilo ni kubwa na kwamba atafikisha kilio cha wananchi hao serikalini.

Alisema kuna uwezekano wanyama hao wamekuwa wengi kwenye hifadhi hiyo kiasi kwamba maeneo yao yamekuwa hayatoshelezi mahitaji hali ambayo inawafanya waingie kwenye mashamba ya wananchi. Kutokana na ongezeko la wananchi katika wilaya hiyo, alisema waliamua kuiomba serikali isogeze mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ili wananchi wapate maeneo kwa ajili ya kilimo na shughuli zingine za kiuchumi.

"Katika hali ya kawaida mtu unaweza ukachanganyikiwa, umetumia gharama kubwa kutunza mazao ukitegemea utavuna halafu mazao yanapotea, inauma sana, mimi kama mwakilishi wenu isingeweza kuingia akilini niendelee na vikao vya bunge wakati wananchi mnakufa njaa," alisema Mtega.

Alisema atawaomba wataalamu wawashauri wananchi hao namna ya kufanya ili kukabiliana na wanyama hao ambao wamekuwa wakisababisha hasara kubwa kwa wananchi na kwamba uharibifu uliofanywa ni ushahidi tosha kwamba maeneo hayatoshi.

Ofisa Maliasili kutoka TANAPA, Helen Mchati, ambaye anaongoza kikosi kazi kilichotumwa na Wizara ya Maliasili na Utalii wilayani humo kuwaondoa tembo hao, aliwataka wananchi hao kuwa watulivu wakati kikosi hicho kikiendelea kufanya kazi.

Mchati aliwataka wananchi hao kutumia pilipili kwa ajili ya kuwafukuza tembo hao kwenye mashamba kama ambavyo wanapatiwa elimu na wataalamu.

Alisema mpaka sasa wameshatimiza siku tano kwenye mashamba hayo wakilinda usiku na mchana huku akiwataka wananchi hao kuepuka kupita mashambani nyakati za usiku kwa maelezo kuwa maofisa hao wanatumia silaha za moto.



Mbunge wa Jimbo la Mbarali mkoani Mbeya, Francis Mtega (kulia), akizungumza na baadhi ya vijana wa Kijiji cha Ihahi, Kata ya Chimala, wilayani humo juzi, alipofanya ziara ya kuangalia namna ambavyo mpunga umekauka mashambani kwa sababu ya kukosa maji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wahofia kuathirika na kemikali za mgodi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKAZI wa Kijiji cha Isoko wilayani Chunya, wameiomba serikali kuwaondoa wachimbaji wadogo wa dhahabu wanaofanya shughuli zao jirani na vyanzo vya maji.

Wananchi hao wamedai kuwa wachimbaji hao wanatumia kemikali ambazo ni hatari kwa afya zao.

Ombi hilo walilitoa juzi wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kwenye kijiji hicho na kusema kemikali zinazotumika kwenye madini hayo zinaingia kwenye maji ambayo wanayatumia.

Mmoja wa wananchi hao, Joshua Mangomango, alisema kijiji kizima kinategemea maji kutoka kwenye chanzo hicho na kwamba hawana uhakika kama maji hayo ni salama kwao kutokana na kemikali zinazotumika.

"Sisi tunachokiomba ni hii mitambo iondolewe hapa ipelekwe sehemu nyingine maana hatuna uhakika kama hizi kemikali haziingii kwenye maji ambayo tunayatumia," alisema Mangomango.

Alisema hawataki mgodi ufungwe kwa sababu hata wao wananufaika kiuchumi, hivyo akaiomba serikali iwasaidie kupima maji ya chanzo hicho ili wajuwe kama kuna kemikali ama la!

Naye Elflahim Kangetile alisema kipindi hiki cha mvua kuna uwezekano mkubwa wa kemikali kuingia kwenye maji na kusababisha madhara kwa maelezo kuwa mitambo hiyo iko jirani mno na chanzo hicho cha maji.

Alisema wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu lakini hakuna mabadiliko yoyote yaliyofanyika zaidi ya shughuli hizo kuendelea kufanyika kwenye eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, alisema sehemu hiyo ni miongoni mwa maeneo wilayani humo ambayo wananchi wamekuwa wakichimba dhahabu kwa amani tofauti na maeneo mengine ya wilaya hiyo.

Alisema katika baadhi ya maeneo kumekuwa na migogoro ya mara kwa mara baina ya wachimbaji wadogo na wakubwa ambao wamekuwa wakigombea maeneo ya kufanyia kazi.

"Hawa wananchi wamekuwa wakifanya kazi zao kwa amani na hata namna wanavyosuluhisha migogoro yao utaona kwamba wanasuluhisha kwa njia ya amani tofauti na sehemu zingine," alisema Mayeka.

Akijibu kero hiyo ya mgodi kuwa katika karibu na chanzo cha maji, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila alisema anasubiri apate ushauri wa kitaalamu ili afanye uamuzi sahihi kwa maelezo kuwa kuna uwezekano jambo hilo likachanganywa na siasa.



# Rais ataka ujenzi kwa huduma bora

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amesema ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal III), katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume unapaswa kwenda sambamba na utoaji wa huduma bora kwa wasafiri.

Dk. Mwinyi aliesema hayo juzi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, alipolitembelea Jengo jipya la Abiria (Terminal III) lililo katika hatua za mwisho kukamilika ujenzi wake.

Alisema ujenzi wa jengo hilo umefanywa ili kuimarisha upatikanaji wa huduma bora kwa wasafiri, hivyo akawataka wasimamizi kuhakikisha kasoro mbalimbali zilizopo zinarekebishwa ili kuwapo utoaji mzuri wa huduma.

Dk. Mwinyi alisema ameridhishwa na hatua iliofikiwa ya ujenzi huo na kuwataka wasimamizi kurekebisha kasoro ndogo ndogo ili kuwa na uwanja wa kisasa na kuepuka hali iliyopo katika jengo la zamani.

Aliyataja maeneo yanayohitaji kushughulikiwa kuwa ni pamoja na kuongeza vizimba vya uhamiaji, eneo la ukaguzi wa mizigo na kuongeza mashine kwa watendaji wa masuala ya forodha.

Pia aliwataka wasimamizi wa ujenzi huo kuhakikisha kunakuwapo mabango yanayoainisha taarifa za safari za ndege kama ilivyo katika viwanja vyote vya kimataifa duniani, jambo ambalo halijafanyika hadi sasa.


Aidha, aliwataka kukamilisha hatua mbalimbali zilizobaki mbele ya jengo hilo, ikiwamo upandaji wa majani, ujenzi wa uzio na barabara ili kuupa haiba uwanja huo, huku akibainisha kuwa sura ya nchi huanzia pale mtu anaposhuka.

Naye Katibu Mkuu Wizara Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Amour Hamil Bakar, alisema ujenzi wa jengo hilo uko hatua za mwisho kukamilika na unatarajiwa kukabidhiwa serikalini mapema mwezi ujao.

**Dk. Mwinyi alisema ameridhishwa na hatua iliofikiwa ya ujenzi huo na kuwataka wasimamizi kurekebisha kasoro ndogo ndogo ili kuwa na uwanja wa kisasa na kuepuka hali iliyopo katika jengo la zamani**

# Mwinyi udugu wa Zanzibar na Oman

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Balozi wa Tanzania nchini Oman, Abdalla Abbas Kilima, Ikulu Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameupongeza uhusiano na ushirikiano mzuri kati ya Zanzibar na Oman na kueleza haja ya kuongeza ushirikiano zaidi katika sekta ya biashara.

Dk. Mwinyi ameyasema hayo Ikulu jijini Zanzibar alipofanya mazungumzo na Balozi wa Tanzania nchini Oman, Abdalla Abbas Kilima, aliyefika Ikulu kwa ajili ya kujitambulisha na kumsalimia Rais. Alisema Zanzibar ina historia nzuri kati yake na Oman na tayari kumekuwa na uhusiano na ushirikiano mzuri katika nyanja mbalimbali lakini ni vyema ushirikiano huo pia ukaimarishwa kwenye sekta ya biashara.

Rais mwinyi alisema Oman ni mdau mkubwa wa maendeleo kwa Zanzibar, hivyo ni vyema uhusiano wa kidugu na wa kihistoria uliopo ukaimarishwa zaidi.

Alitoa pongezi kwa serikali ya Oman kwa kuonyesha utayari wa kusaidia ukarabati wa majengo ya kale ya Beit al Ajaib na Jumba la Wananchi Forodhani ambapo mchakato wake unaendelea.

Kuhusu ujenzi wa bandari, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetiliana saini hati ya makubaliano na Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman inayohusu mpango mkuu wa ujenzi wa bandari ya Mangwapwani/Bumbwini na kuigeuza bandari ya Malindi kuwa ya kitalii na kwamba serikali iko tayari katika ushirikiano huo na serikali ya Oman.

Rais Mwinyi alitoa shukrani kwa utayari wa kampuni hiyo kwa kufanya upembuzi yakinifu kwa fedha zake yenyewe pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ya Oman kwa kuonyesha nia ya kushirikiana na Zanzibar kwa azma ya kuwekeza katika viwanja vya ndege Unguja na Pemba.Sambamba na hayo, Rais Mwinyi alisisitiza haja kwa serikali ya Oman kutoa fursa katika kupata soko la bidhaa za Zanzibar nchini humo kwa kua soko la ukanda wa ghuba limekuwa na uzoefu na historia kubwa ya bidhaa za Zanzibar.

Pia alieleza haja ya kuwapo kwa soko la uhakika la bidhaa za Zanzibar nchini Oman zikiwamo za matunda, mwani, viungo na karafuu hasa ikizingatiwa kwamba bei ya dunia ya karafuu imekuwa ikishuka hivi sasa.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi alieleza hatua ya ushirikiano uliopo kati ya Zanzibar na Oman na kueleza Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman ilivyotiliana saini na Zanzibar katika Mpango Mkuu wa Ujenzi wa Bandari ya Magapwani/Bumbwini.

Naye Balozi Kilima alisema serikali ya Oman imekuwa na uhusiano mwema na wa kihistoria na Tanzania ikiwemo Zanzibar na kueleza hatua ambazo Oman inaendelea kushirikiana na Zanzibar ikiwamo ukarabati wa majengo ya kihistoria.

Aliahidi kulifanyia kazi suala la biashara kati ya Zanzibar na Oman hasa ikizingatiwa kwamba tayari kuna Baraza la Biashara ambalo liliundwa kwa ajili ya ushirikiano katika sekta hiyo baina ya nchi hizo mbili.

# Hemed awataka viongozi kutafuta mbinu zaidi kutatua kero za watu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleimana Abdulla, amesema viongozi wa taasisi za umma waliopewa jukumu la kuwahudumia wananchi lazima wajiongeze katika kutafuta mbinu mbadala zitakazosaidia kuwaondoshea usumbufu katika maisha yao ya kila siku.

Akimalizia ziara zake za kutembelea wilaya zote za Unguja na Pemba kwa Wilaya ya Mjini juzi na kukagua shughuli za maendeleo na kutafuta mbinu za kukabiliana na changamoto zinazowakabili wananchi, alisema kero zinazoizunguka jamii katika maeneo yao, lazima zitafutiwe suluhisho la haraka na la kudumu.

Makamu wa Rais alisema ubovu wa barabara, akitolea mfano wa ile iliyoanzia Darajani, Karo Bovu pembezoni mwa duka la Suma, alisema uchafuzi wa mazingira katika maeneo mengi ya manispaa bado vinaendelea kusumbua wananchi hasa wafanyabiashara na wageni wanaotembelea mji kupata huduma za Kibiashara.

Hemed alitoa mwezi mmoja kwa uongozi wa Manispaa ya Mjini kuifanyia matengenezo barabara hiyo hata kwa hatua ya kifusi pamoja na karo zinazomwaga maji machafu katika eneo la Suma ambalo ni kitovu cha biashara. Aliagiza kazi hiyo lazima iende sambamba na marekebisho ya maeneo yanayotuama maji ya mvua yaliyoko pembezoni mwa uwanja wa michezo wa Malindi na Mchangani yasiyoleta haiba nzuri hasa kwa wageni wanaotembelea visiwa vya Zanzibar. Makamu wa Pili wa Rais alisisitiza kuwa wilaya ya Mjini lazima iwe mfano bora katika makusanyo ya mapato kutokana na kuwa na vyanzo vingi vya mapato ikilinganishwa na wilaya zingine ili baadaye yatumike kuimarisha miundombinu ya miradi ya wananchi.

Alisema nchi inakusudia kwenda kwenye uchumi uliokomaa, hivyo ni vyema viongozi na watendaji wa umma wakazingatia kufanya kazi kwa bidii katika kutoa huduma za kijamii kama mahitaji ya wananchi yanavyojionyesha kila wakati.

Akizungumza na wafanyabiashara wadogo katika soko la Darajani, Hemed alisema kwa kuzingatia umuhimu wao, serikali imetenga eneo mahsusi la Kibandamaiti ili liwasaidie kupata kipato cha kukidhi mahitaji yao pamoja na kusaidia uchumi wa taifa.

Hemed alisema maandalizi ya kuweka mazingira bora ya kibiashara ndani ya soko hilo kwa sasa yamekamilika ndiyo maana uongozi wa wilaya kwa kushirikiana na Manispaa ya Mjini, imesharuhusu kuanza kwa soko hilo hivi karibuni.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA INA VYUMBA VIWILI IPO KIJITONYAMA PLOT NAMBA 712/1 BLOCK 46 DAR ES SALAAM BEI 300M,MAZUNGUMZO YAPO.

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi**
**Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

DEOCARA BARNABAS WA NGARA KAGERA ANATANGAZA KUPOTEZA KADI YAKE YA PIKIPIKI AINA YA SKYMARK YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 691 CQB, INJINI NAMBA 162FMJ-B20A01483 NA CHESISI NAMBA LAEE1CCJXLMA01546. YEYOTE ATAKAYEIONA AIPELEKE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU APIGE SIMU NAMBA 0768371591 AU 0755258959.
TAARIFA IMETOLEWA KITUO CHA POLISI KWA NAMBA NGR/RB/793/2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MULEBA MKOA KAGERA**
**MAOMBI NA. 35/2021**
**AGNESI DEOGRASIAS ................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1. VEDASTO DEOGRASIAS**
**2. ANATOLI KALAGANO .............WAJIBU MAOMBI**

KWA:
VEDASTO DEOGRASIAS (POPOTE PALE ULIPO)
Unaarifiwa kuwa Maombi Na. 35/2021 yamepangwa kutajwa tarehe 14/05/2021 Mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, J.K. Banturaki saa 2:30 asubuhi, mahali - Muleba (Mamlaka ya Mji Mdogo).
Hivyo, unaamriwa kuhudhuria mwenyewe / mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 09/04/2021.

..........................................
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MULEBA**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.108/2021**

Ombi la **FELISTA BENARD** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **DENIS UJENI KIJELI**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 18/05/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 15/04/2021**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.109/2021**

Ombi la **ROSE JOHN KESSY** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **DENIS ALPHONCE TEMU**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 22/04/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 15/04/2021**

## TANGAZO LA KUFUNGA BIASHARA BRELA .

**MOHAMEDRAZA HUSSEIN JETHA**
DIRECTOR
GUEST SUPPLIES.
P.O.BOX 7114
ARUSHA.
SIMU: 0754 269 370
ANATANGAZA KUFUNGA BIASHARA YA GUEST SUPPLIES
YENYE TIN NO 105-084-730.
ILIYOSAJILIWA BRELA KWA NAMBA 287207
MWAKA 2019 ARUSHA CBD .

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**AIR TRAVEL TOUR LTD**
WANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI
**T167 APJ TOYOTA**
LANDCRUSER
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI :
**ARU/ARU/RB/190104/2021**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA KILOSA**

**S.L.P.29**
**KILOSA**
**01.04.2021**

**YAH: MAOMBI YA RUFAA NA.20/2021**

**HAPPINES W.HASSANI..................... MLETA RUFAA**

**DHIDI YA**

**JOFULEI H.MMASI........................ WAJIBU RUFAA**

**WITO WA KUITWA SHAURINI KWA JOFULEI H.MMASI**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya kilosa,
Tarehe 30/06/2021 mwenyewe binafsi au muwakilishi wako bila kukuosa ambapo maombi yamepangwa kusikilizwa.Endapo hutahudhuria, rufaa yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.
Imesainiwa Leo tarehe 01 mwezi 04 mwaka 2021.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO**
**Usimamizi wa mirathi 19 /2021**
**Ombi la RAMADHAN HASSAN kuteuliwa kuwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu ISSA RAMADHANI HASSAN**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 28/04/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa. Tarehe 14/04/2021




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

## NOTISI / TANGAZO

**NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili. Vinginevyo, tutafanya mnada wa hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| NA | JINA LA MDAIWA | TAWI ALILOKOPA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | TAREHE NA SAA YA MNADA | MAHALI DHAMANA ILIPO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | SHAIBU SAID MGANDILWA | CT NO. 1692, PLOT NO.1134, BLOCK "M" | 03/05/2021 SAA 3:30 ASUBUHI NA KUENDELEA | FOREST -MBEYA L.R |
| 1. | MAHAWI ENTERPRISES LIMITED | UKONGA | JOSEPH ELIUTHER MAHAWI | CT NO. 31358, PLOT NO. 1369 BLOCK NO. "A" | 08/05/2021 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA | NORTH BUSWELU-MWANZA |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika. Na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754 497 396 / 0752 000 695
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

## GSP AUCTION MART

P.o.Box 31088 Dar es Salaam
Tanzania, Tel: + 255 687 638679 +255 654 922892
Sinza Africasana near by sokoni Africasana Block No. 31
Email: gsp.recovering@gmail.com / gsp.recovering@outlook.com

**KUMB No. AFCL/2021/DM/020**
**GSP AUCTION MART** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** S.L.P 40780 Dar es salaam tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Ijumaa tarehe 30/04/2021 mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai Mabatini.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| MOSES PETER ABDONI | LP 909 BUS | T877 DNN | DAR ES SALAAM |
| ABDALLAH KIBWANA KIBWANA | LP 909 BUS | T351 DPS | DAR ES SALAAM |
| BASHIR LEONI MSIMBE | LP 909 BUS | T163 DNT | DAR ES SALAAM |
| BASHIR LEONI MSIMBE | LP 909 BUS | T164 DNT | DAR ES SALAAM |
| HEKIMA GERVAS BIDYANGUZE | LPO 909 | T421 DRX | MWANZA |
| HEKIMA GERVAS BIDYANGUZE | LPO 909 | T763 DRX | MWANZA |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T678 DNE | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T613 DMQ | DAR ES SALAAM |
| GREPHSON BARIKIEL SHOO | LP 909 | T367 DSR | DAR ES SALAAM |
| GREPHSON BARIKIEL SHOO | LP 909 | T308 DSR | DAR ES SALAAM |
| SHABAN RAJABU SOUD | LP 909 BUS | T615 DQF | DAR ES SALAAM |
| SHABAN RAJABU SOUD | LP 909 BUS | T790 DRD | DAR ES SALAAM |

1. Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**
**GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM.**
**+255 654 922 892, +255 687 638 679**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MAHOJIANO MAALUM

# Msekwa afunguka kuhusu Samia-2

**Na Romana Mallya**



Jana katika mahojiano yetu na mwanasiasa mkongwe nchini, Pius Msekwa, ambaye aliwahi kushina nafasi mbalimbali za uongozi wa chama na dola, alielezea mambo kadhaa kuhusiana na mtazamo wake kwa Rais Samia Suluhu Hassan, yakiwamo uteuzi wa makatibu wakuu, nyayo za Hayati Rais Magufuli, taaluma za wateule, utawala bora na katiba mpya. Fuatilia sehemu ya pili na ya mwisho.

**MWENYEKITI CCM**

Akimzungumzia Rais Samia katika nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Taifa na mabadiliko ndani ya chama, Msekwa anasema kubadilisha chombo ambacho kiongozi mpya anaingia, kunategemea na mtazamo na mwekeleo wa mhusika.

"Anataka mambo yaende vipi, huwezi kubashiri mapema, huwezi kupiga ramli, ukasema atabadilisha. Ninavyoona sasa hivi CCM inakwenda vizuri, tuliisuka tangu tulivyokuwamo, nikiwa Katibu Mkuu Mtendaji wa CCM na mwanzilishi haswaa, CCM tuliisuka vizuri na Mwalimu Julius Nyerere (Baba wa Taifa).

"Tuliisuka kimfumo, kitaratibu, kikanuni, kwa hiyo kukosoa mfumo uliopo umeendelea hivyo hivyo tangu mwaka 1977 hadi leo, kufumua kutokana na upungufu ni ngumu, kitu kilichosukwa vizuri kikafanya kazi kwa muda wote huo, sana sana atabadilisha watu wa kuendesha, ambao lazima wabadilike kwa sababu kuna uchaguzi kila baada ya miaka mitano.

"Na uchaguzi ndani ya CCM utafanyika mwaka ujao (2022), haya mabadiliko yatakuwapo lakini mfumo wa uendeshaji na kanuni au Katiba yake nafikiri yatabaki kama yalivyo, sina ninachokiona kinastahili kubadilishwa."

**RIPOTI YA CAG**

Msekwa ameshauri mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere yaliyowasilishwa bungeni (Aprili 8) ambayo yamebainisha dosari nyingi, yafanyiwe kazi.

"Mapendekezo yake yafanyiwe kazi, yamekuwa yakifanyiwa kazi miaka yote, lakini kwa sababu huo ni utaratibu wa katiba, CAG anatoa taarifa yake kwa Rais na naye anaipeleka bungeni, na miaka yote tulikuwa tukifanya hivyo.

"Rais akishakabidhi taarifa kwa Spika inajadiliwa bungeni na kasoro zinajadiliwa na maelekezo yanatolewa na Bunge namna ya kurekebisha, mengine yanasikilizwa mengine yanadharauliwa na watendaji, lakini huo ndiyo ubinadamu ulivyo," anasema.

**NGORONGORO IPUNGUZWE**

Anasema anaungana na Rais Samia kuhusu wasiwasi wake dhidi ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro kwamba anaona kuna ugumu wa kuiendesha kutokana na wingi wa watu waliomo.

"Kwa bahati nimewahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa miaka sita mfululizo wakati wa utawala wa Rais Kikwete ambaye aliniteua, ukubwa wa hifadhi hii ni kilomita za mraba zaidi ya 8000, hili ni eneo kubwa sana lililoundwa wakati ule, mwaka 1959.

"Nafikiri eneo lote lilikuwa ni pori halina watu, na watu waliokuwamo nasikia walikuwa 8,000 wakati huo, leo wanakaribia 100,000 lakini wanaishi eneo hilo hilo, halafu kuna sheria kali zinawazuia wasilime mazao ya chakula."

Anasema wamasai wa mwaka 1959 walikuwa wanaishi kwa maziwa pekee tofauti na wa sasa, wanataka vyakula vingine huku sheria ikiwataka wasilime wategemee chakula cha kununua au cha msaada.

"Naungana na Rais na kupendekeza eneo hilo lipunguzwe ukubwa wake na ibakie mita za mraba 200 ambazo ni Bonde la Ngorongoro (Creator) na misitu iliyo karibu yake."

"Lazima tukubali ukweli watu wataendelea kuishi kule, dawa ni kuondoa neno hifadhi katika vijiji vile ili vibaki kuwa vijiji vya kawaida kama vya Maswa, yapo maeneo ya mbali na hapo yanaitwa Katesio ambayo ni kilometa nyingi ambako ukienda hukutani na mnyama yoyote zaidi ya binadamu na ng'ombe wa kufuga."

Anasema anadhani wakati umefika wa kufikiria kupunguza eneo lile libaki bonde lenyewe lenye wanyama wengi ambalo linatunzwa vizuri na lina kamera maalum ambazo hata alipokuja Rais mstaafu wa Marekani, Bill Clinton, alitembezwa kupitia mfumo huo unaoelekeza wapi wanyama walipo.

"Kama ningeombwa ushauri kuhusu hifadhi ya Ngorongoro ningeshauri vijiji hivi vya wamasai tuachane navyo," anasema.

**MFUMO WA VYAMA VINGI**

Mfumo wa vyama vingi unataka baada ya uchaguzi ushindani uhamie ndani ya Bunge.

Nikiwa Spika wa Bunge mwaka 1993, nilihamisha Bunge kutoka katika chama kimoja na kuwa la vyama vingi kupitia uzoefu wa tuliowaiga ambao ni Waingereza.

Kama upinzani unaonekana umelala hayo ni makosa yao wenyewe na hakuna wa kulaumiwa.

Bungeni tumeweka utaratibu mzuri na kanuni za kuwawezesha kufanya kazi nzuri, wasilale lale wafanye kazi kulingana na utaratibu tuliowawekea, wakati wa uchaguzi wafanye kazi. Wananchi waliamua wanaridhika na kazi za Magufuli, wakawaweka pembeni, wakampa Magufuli wabunge wote, kanuni zinawaruhusu waamke," anasema

.

**MSEKWA NI NANI**

Kabla ya kuwa Spika wa Bunge kwa miaka 15, kuanzia mwaka 1994, alifanya kazi nyingi za taifa, alikuwa Katibu wa Bunge, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mkuu wa Mikoa ya Tabora na Kilimanjaro.

Katika utumishi wake wa umma, aliumalizia katika Ofisi ya Waziri Mkuu, akiwa Katibu Mkuu wa Waziri Mkuu.

"Nimepita katika uzoefu mwingi katika utumishi wa umma kwa ngazi ya taifa, lakini inayojulikana zaidi ni hii ya Spika wa Bunge mstaafu," anasema.

Akiwa ndani ya Bunge, alikuwa Spika mwenye bahati ambaye amekaa kwenye kiti hicho kwa muda mrefu wa miaka 15.

"Nikiwa Naibu Spika miaka minne ya kwanza, Spika wa Bunge, alikuwa ni Adam Sapi, lakini bahati mbaya afya yake ilikuwa imedhoofu sana kwa hiyo alikuwa akiniachia kuongoza shughuli za Bunge kila siku.

"Nilirithi kiti chake na miaka 11 iliyobaki nikawa Spika wa Bunge, nikapata uzoefu wa kutosha kuendesha shughuli hizo."

**MTAZAMO BUNGE LA SASA**

Akilinganisha na yaliyopita, Msekwa anasema inategemea mtu analinganisha mambo gani kwa sababu katika shughuli za Bunge zilizowekwa kikatiba hazina tofauti.

"Ukilinganisha majukumu ya Bunge hayana tofauti hata kidogo, kilicho tofauti peke yake ni wabunge, hawa ni binadamu wanabadilika, kila miaka mitano wanachaguliwa watu wengine na zaidi wanakuwa ni vijana, wenye ari mpya na kasi mpya, michango yao bungeni ndiyo inabadilika, kulingana na waliokuwapo wakati ule nikiliongoza," anasema.



# HAALAND HAZUILIKI, ASEMA GUARDIOLA

**DORTMUND, Ujerumani**

ERLING Haaland "hazuiliki" kwa mujibu wa Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, licha ya kikosi chake kumzuia nyota huyo wa Borussia Dortmund kutowafunga kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

City walifuzu hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza chini ya Guardiola kwa kipindi cha miaka mitano aliyokaa hapo, baada ya Riyad Mahrez kufunga kwa penalti na Phil Foden kufunga goli la pili dakika ya 75.

Mabao hayo mawili yalizima lile la kwanza la Jude Bellingham na hivyo kufanya mchezo huo kumalizika kwa 2-1 na City wakasonga mbele kwa ushindi wa uwiano wa mabao 4-2.

Haaland alizuiwa vizuri na ukuta wa City na hivyo kushindwa kuleta hatari yoyote.

Na Guardiola akasema baada ya mchezo huo kwamba, kumzuia Halaand kuliwafanya wakae salama zaidi.

"Naweza kusema mchezaji huyo ni kama hazuiliki na njia nzuri ya kuwazuia wachezaji hawa wenye vipaji ni kutowaruhusu kuwa na mpira," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Wanataka mpira, wanahitaji mpira, hivyo usiwaruhusu kuwa nao. Kwa hilo tunahitaji kucheza mpira mzuri na kujaribu kuwaacha wazurule. Na ilitokea kwenye mechi zote mbili. "

City itacheza na PSG kwenye hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa, ambapo msimu uliopita walitinga fainali.

# UNITED YATANGAZA KUMWANIA RICE



**LONDON, England**

NYOTA wa Timu ya Taifa ya England, Declan Rice anawaniwa na Manchester City kutoka West Ham, kwa mujibu wa Manchester Evening News.

Rice mwenye umri wa miaka 22 alizungumza na wachezaji wa United mwezi uliopita wakati wakiwa kwenye majukumu ya Timu ya Taifa, huku England ikishinda mechi zake tatu za kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar.

Mashetani Wekundu hao wanajitaki kiungo, kwani hawana uhakika wa kumbakiza, Paul Pogba mwishoni mwa msimu huu.

Wakati akiwa kwenye majukumu ya Timu ya Taifa, Rice alizungumza na nahodha wa United, Harry Maguire na Luke Shaw kuhusu hali ilivyo ndani ya klabu hiyo.

Mkataba wa Rice wa sasa na wagonga nyundo hao wa London unamalizika ifikapo mwaka 2024, lakini anweza kupatikana kwa bei nafuu zaidi.

Kocha wake, David Moyes amesema Rice anaweza kufikia thamani ya pauni milioni 100 kama klabu yoyote itamtaka.

Lakini kutokana na kuyumba kwa uchumi kwa klabu zote barani Ulaya kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona, anaweza kupatikana kwa bei rahisi zaidi.

# MADRID INATAKA ZAIDI – ZIDANE

**LIVERPOOL, England**

ZINEDINE Zidane amesema Real Madrid inataka zaidi baada ya kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku pia wakipambana kutetea taji la Ligi Kuu Hispania maarufu LaLiga.

Madrid walifuzu nusu fainali hiyo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2018 baada ya kutoka suluhu na Liverpool ugenini na hivyo kuwafanya watinge hatua hiyo kwa uwiano wa mabao 3-1.

Los Blancos, ambao wamepitwa pointi moja na wapinzani wao wa jiji moja, Atletico Madrid kwenye msimamo wa LaLiga , huku zikiwa zimebakia mechi nane, wamefuzu hatua ya nusu fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya kwa mara ya 30, mara 10 zaidi kuliko timu nyingine yoyote na sasa watakutana na Chelsea.

Zidane aliiongoza Madrid kushinda taji hilo mara tatu mfululizo kati ya mwaka 2015 na 2018.

Na baada ya kuwaondoa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England, Liverpool, Mfaransa huyo alisema: "Tunapambana



pamoja na kikosi hiki kinafanya kinachotakiwa na mara zote kinataka zaidi.

"Bado hatujashinda chochote, lakini tupo hai kwenye mashindano ya Ulaya na kwenye LaLiga."

Bila ya uwepo wa nahodha wake, Sergio Ramos na Raphael Varane pale Anfield - Madrid walinufaika na umakini mdogo wa wachezaji kama Mohamed Salah, Georginio Wijnaldum na Roberto Firmino ambao walipata nafasi lakini walishindwa kuzitumia.

Madrid sasa itacheza na Chelsea kwenye hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Ferdinand aishangaa Liverpool

**MANCHESTER,** England

BEKI wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand, amesema bado anajiuliza kuhusu anguko la Liverpool kwa msimu huu chini ya Kocha, Jurgen Klopp.

Liverpool imekuwa kwenye mwendo wa kusuasua msimu huu baada ya msimu uliopita kuwa bora na iliweza kutwaa taji la Ligi Kuu England ambalo kwa sasa inaonekana wazi kwamba inalipoteza kwa sababu ipo katika nafasi ya sita na pointi zake 52 wakati vinara Manchester City wana pointi 74.


Klopp ameondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Real Madrid baada ya kushindwa kupindua meza kwenye robo fainali ya pili pale Uwanja wa Anfield kwa kutoka sare, huku mchezo wa kwanza wakiwa walipoteza kwa kufungwa mabao 3-1.

Beki huyo amesema kuwa bado haelewi ambacho kinaisumbua Liverpool kwa sasa na anadhani labda wachezaji wamekuwa wakicheza chini ya kiwango ama majeruhi yanaitesa timu hiyo.

"Kuna maswali ambayo tumekuwa tukijiuliza kwa nini Liverpool imekuwa inafanya namna hii, labda inaweza kuwa sababu ya aina ya mbinu za mwalimu Klopp? Amekuwa na timu kwa miaka minne, mitano hivi hivyo anawajua wachezaji wake.

"Labda kuna mambo ambayo hayapo sawa itakuwa ni msimu mbaya tu ama kukosa wachezaji wake muhimu kikosini kwa kusumbuliwa na majeraha?

Kwa sasa Liverpool yenye mshambuliaji Mohamed Salah inapeleka nguvu kwenye Ligi Kuu England ili kutetea taji lao.



# KEAN
## azigonganisha Juventus, Milan




**TURIN,** Italia

JUVENTUS na Inter Milan zipo kwenye mtifuano wa kuwania saini ya straika wa Timu ya Taifa ya Italia, Moise Kean, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo kule PSG.

Kean alijunga na miamba hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, kwa mkopo akitokea Everton Oktoba, mwaka jana lakini nyota huyu alikiri kuwa bado hana uhakika kuwa ataichezea klabu gani msimu ujao.

Kwa mujibu wa Tuttosport, Juventus ambayo ni klabu yake ya zamani na Inter Milan wamemweka nyota huyu kuwa kipaumbele kuelekea msimu wa ujao wa 2021-22.

Taarifa zinasema kuwa Inter wao wanajiandaa kufanya dili la mabadilishano na Everton ambalo litamhusisha Matias Vecino na malipo ya ziada ya fedha.

Wakati huo, Juventus wao wakiripotiwa wapo tayari kumwondoa Merih Demiral kwa ajili ya Kean, na wanatajwa kuwa wanampa kipaumbele nyota huyo kuliko Sergio Aguero, ambaye anatarajia kuondoka Manchester City baada ya kumaliza mkataba wake.

Kean ni zao la shule ya soka ya Juventus, na alikamilisha uhamisho wake kuelekea Everton mwaka 2019 kwa euro milioni 30.

Amefunga mabao 18 katika mechi 37 za mashindano yote akiwa na PSG msimu huu.

# Neymar afunguka kuhusu mkataba mpya

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Timu ya Taifa ya Brazil, Neymar amesema suala la mkataba wake mpya na PSG sio tatizo kwa sasa, kwa mujibu ESPN Brazil.

Neymar ameelezea kuwa ana furaha kubwa sana ndani ya klabu hiyo kwa sasa kuliko wakati mwingine wowote.

Straika huyo wa kimataifa wa Brazil ameibuka na kusema hayo baada ya PSG kufuzu hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kuwatoa Bayern Munich ambayo ilikuwa bingwa mtetezi wa taji hilo.

Nyota huyo, ambaye aliwasili PSG akitokea Barcelona kwa euro milioni 222 mwaka 2017, mkataba wake wa sasa unafika mwisho mwakani.

Pande zote zilitajwa kuwa kwenye majadiliano ya mkataba mpya, hadi pale Neymar aliporipotiwa kusitisha mazungumzo ya mkataba mpya.

Nyota huyo alikuwa anahusishwa na kurejea LaLiga, lakini PSG wao wamesisitiza kuwa Neymar hatakuwa sokoni, hata kwa fedha nyingi, kwani hawako tayari kumuuza kwa sasa.

Hata hivyo, alipoulizwa juu ya hali yake ya mkataba mpya amebainisha hilo sio tatizo kwa sasa.

Akizungumza na ESPN Brazil amenukuliwa akisema; "Kusaini mkataba mpya, sio tatizo kwa sasa kwa upande wangu.

"Kimsingi nahisi kuwa huru na kuwa nyumbani hapa PSG. Nahisi kuwa na furaha kuliko wakati mwingine wowote."

***



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TIKETI LIGI YA MABINGWA ULAYA INAMVURUGA KLOPP

### Kocha huyo asema timu yake itapambana kuhakikisha inamaliza katika 'Top Four' ili...

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amebakia anajiamini Liverpool inaweza kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, ingawa anafahamu mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England wanatakiwa kupambana ili kumaliza kwenye nne bora.

**Liverpool ilishindwa kufuzu nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kutoka suluhu na Real Madrid juzi Jumatano na hivyo kutolewa kwa uwiano wa mabao 3-1.**

Liverpool ya Klopp ilipiga mashuti 13 kwenye lango la Real Madrid, lakini hawakuweza kufunga bao lolote dhidi ya mabingwa hao wa LaLiga.

Huku matumaini ya Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya yakiwa yamefikia mwisho, wekundu hao sasa watatakiwa kupambana kwenye Ligi Kuu England ili kuhakikisha wanamaliza kwenye nne bora, ambapo kwa sasa wapo nafasi ya sita katika msimamo wa ligi hiyo, wakipitwa pointi tatu na West Ham waliopo nafasi ya nne.

"Hakuna cha kufanya kuhusu kujiamini, naweza kusema kujiamini ni asili tu, lakini hiyo haina maana tutamalizia tukiwa pale," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo dhidi ya Madrid.

"Tunaweza kusoma msimamo, tunajua pointi zilizopo, tunajua hali ilivyo kwa sasa kwa upande wetu.

"Tunajua nani tunacheza nae na hatuwezi kuzungumza sana kuhusu hilo, nasema kwamba kwa sasa tunafikiria sana kuhusu hilo.

"Hata hivyo, tunatakiwa kupambana sana ili mambo yaweze kwenda kama tulivyopanga na tunatakiwa kumaliza kwenye nne bora ili kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

"Nafikiri hatupo kwenye wakati mbaya kwa sasa; tulicheza vizuri na hata kwenye mchezo wetu wa ushindi dhidi ya Aston Villa. "Tulicheza mchezo mzuri dhidi yao, tulicheza pia vizuri dhidi ya Arsenal na tukacheza vizuri sana dhidi ya Real Madrid kwenye mchezo wa kwanza, lakini mchezo huu mwingine hatukuwa vibaya sana.

"Usiku huu (juzi) tulikuwa na mchezo mzuri na tunatakiwa kuendelea kusonga mbele kwa kupambana.

"Tunatakiwa kupambana sana, kwa sababu tunatakia kuwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, na tunatakiwa kupata pointi nyingi kuliko timu nyingine."

## KWA UFUPI

**LINGARD HAJUI HATIMA**

KIUNGO wa kati wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28, hajaamua kuhusu ikiwa anataka kurejea Manchester United baada ya kucheza vyema kwa mkopo kule West Ham. (***Goal***)

**RICE ANUKIA UNITED**

KIUNGO wa West Ham United na England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, anataka kujiunga na Manchester United. (***Manchester Evening News***)

**LENO NJIA MOJA**

GOLIKIPA wa Arsenal na Ujerumani, Bernd Leno mwenye umri wa miaka 29, anasema "yuko wazi kwa mapya" na kwamba hapajawa na mazungumzo ya kurefusha mkataba wake na washikabunduki hao. (***Times - subscription required***)

**BARCA YAKOMAA NA HAALAND**

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, ni mchezaji anayelengwa zaidi na Barcelona kwa sasa. Timu hiyo ya Hispania inataka kumsajili wakati wa dirisha la uhamisho wa kipindi cha majira ya joto. (***Mundo Deportivo***)

**GARCIA AKARIBIA BARCA**

BARCELONA wanaamini kuwa watakamilisha uhamisho wa mlinzi wa kati wa Manchester City na Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 20, kufikia mwisho wa mwezi huu. (***Sport***)

**JUVE KUMREJESHA KEAN**

JUVENTUS inataka kumsajili tena mshambuliaji wa Everton na Italia, Moise Kean, ambaye anacheza kwa mkopo kule Paris St-Germain. Everton wanataka euro milioni 50 kwa ajili ya kumwachia nyota huyo mwenye umri wa miaka 21. (***Gazzetta***)

**CHELSEA, JUVE ZAJIPANGA**

CHELSEA wanaangalia uwezekano kubadilishana wachezaji kati ya Alex Sandro mwenye umri wa miaka 30 kutoka Juventus na Emerson Palmieri mwenye umri wa miaka 26 kwenda jijini Turin. (***Calciomercato***)

**BERNARD KUTUA BETIS**

WINGA wa Everton, Bernard mwenye umri wa miaka 28, anawaniwa na kocha wa Real Betis, Manuel Pellegrini na anataka kumsajili wakati wa dirisha la uhamisho la kipindi cha majira ya joto kinachokuja. (***Fichajes***)

**BARKLEY HAKIJAELEWEKA**

ASTON Villa wameiambia Chelsea kuwa hawana haja na mkataba wa kudumu na kiungo wa kati wa England, Ross Barkley mwenye umri wa miaka 27 ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo. (***TEAMtalk***)

**CAMAVINGA SOKONI**

LIVERPOOL wanaweza kusaini mkataba na kiungo wa kati wa Rennes na Ufaransa, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 18, msimu huu kuziba nafasi ya Georginio Wijnaldum (30), ambaye yuko tayari kuondoka wakati mkataba wake utakapokwisha. (***Express***)

## HABARI MICHEZO

# TIKETI KOMBE LA DUNIA YAMPAGAWISHA PAWASA

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya ufukweni kimeingia kambini jana kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon Beach-Soccer), zinazotarajiwa kufanyika kuanzia Mei 23, mwaka huu nchini Senegal.

Tanzania ilikata tiketi ya kushiriki fainali hizo baada ya kuiondoa Burundi kwa jumla ya mabao 12-9.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pawasa alisema kikosi chake kitaendelea na programu maalumu aliyoiandaa ili kukifanya kuwa imara kwenda kupambana kwenye fainali hizo.

Pawasa alisema wachezaji wake watafanya mazoezi kwa kufuata programu hiyo iliyogawanya katika awamu tatu na anaamini itawajenga kwenda kukabiliana na ushindani kwenye michuano hiyo.

Alisema wiki ya kwanza itakuwa ni kwa ajili ya mazoezi ya kuwaweka fiti na utimamu wa mwili na baadaye watahamia kwenye mazoezi ya kiufundi, mbinu, ujanja na ubunifu.

"Wiki ya tatu tutamalizia kwa kucheza mechi za kirafiki, tunahitaji kupata mechi tano ambazo zitatupa nafasi ya kujitathimi na kuona mapungufu yetu kabla ya kwenda kwenye fainali hizo,".

"Malengo yetu makubwa katika fainali hizo ni kufanya vizuri na kuwa miongoni mwa timu kutoka bara la Afrika zitakazokwenda kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika nchini Urusi Septemba, mwaka huu,"alisema Pawasa.

Aliongeza anahitaji kuita wachezaji wengine wawili kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kikosi chake kuelekea fainali hizo.

Tanzania imefuzu kucheza fainali hizo za ufukweni kwa mara ya kwanza baada ya kuiondoa Burundi iliyotumia ufukwe wa Coco jijini kama uwanja wake wa nyumbani mapema mwezi huu.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mahusiano wa Benki ya Standard Chartered, Juanita Mramba (kulia), akipiga mpira katika uzinduzi wa shindano jipya ambalo mshindi wa jumla atapelekwa nchini England kutembelea Uwanja wa Anfield unaomilikiwa na timu ya Liverpool. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa benki hiyo, Ajmair Raiz, **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtaturu aing'ata sikio Simba SC

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Singida Mashariki, (CCM), Miraji Mtaturu ameshauri kuongezwa maneno katika jezi za mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba na kuwa Visit Tanzania,The Land of Kilimanjaro and Zanzibar ili kuvutia watalii wengi zaidi kuingia hapa nchini.

Simba ambao ni wawakilishi pekee wa Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, inatumia nembo ya Visit Tanzania katika michuano hiyo kutokana na mdhamini wake SportPesa kukinzana na kampuni nyingine yenye nmakubaliano na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Akichangia bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2021/22, Mtaturu alisema lengo la kufanya hivyo ni kuwaonyesha watalii vivutio vilivyopo Tanzania.

"Leo hii Simba wanasema Visit Tanzania, Mimi naomba niongeze tuseme Visit Tanzania,The Land of Kilimanjaro,Serengeti and Zanzibar ili wanapoenda kwenye robo fainali dunia nzima ione vivutio tulivyonavyo," alisema mbunge huyo.

Katika hatua nyingine, Spika wa Bunge, Job Ndugai ametangaza uongozi mpya wa michezo wa Klabu ya Bunge ambapo Mbunge wa Kinondoni (CCM), Abbas Tarimba amechaguliwa kuwa Mwenyekiti huku makamu wake akiwa ni Mbunge wa Viti maalum, Esther Matiko.

Wengine waliochaguliwa ni Meneja wa timu hiyo, Seif Gulamali na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ni Ridhiwani Kikwete, Aeshi Hilaly, Stanslaus Mabula, Anna Lupembe na Rose Tweve.

## HITIMANA AAMUA KUITOSA MTIBWA

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Thiery Hitimana amesema hafikirii kurejea nchini hadi msimu ujao utakapofika, licha ya kupata kupata ofa kutoka katika timu nyingine inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Hitimana aliliambia gazeti hili baada ya kusikia kauli Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru kwamba uongozi wa klabu hiyo umeanza mchakato wa kumtumia nauli ya ndege ili arejee nchini kuendelea na majukumu yake hadi mwisho wa msimu huu.

Kocha huyo alisema baada ya kuondoka Mtibwa Sugar alipata ofa ya timu moja ya Rwanda na nyingine ya Tanzania lakini amezikataa na kuhitaji kupata muda wa kumpumzika.

"Sio kweli kwamba viongozi wananitumia tiketi ili nirejee katika majukumu yangu, nimepata ofa ila nimapema kuweka wazi timu ambayo imenifuata, lakini niliwaambia kwa sasa nahitaji kupumzika, hivyo wakinihitaji tusubiri hadi msimu ujao," alisema Hitimana.Alisema alifikia uamuzi huo ili kutoweka rekodi ya kufundisha tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara ndani ya msimu mmoja.

Kocha huyo wa zamani wa Namungo FC ameamua kuachana na Mtibwa Sugar baada ya kutokuwa na maelewano na msaidizi wake, Vincent Barnabas.

## STANDARD CHARTERED KUWAENZI WAHANGA

**Na Enock Charles**

KATIKA kukumbuka tukio janga la Hillsborough lililopelekea watu 96 kufariki dunia katika mchezo wa nusu fainali kati ya Liverpool dhidi ya Nottingham Forest za England, benki ya Standard Chartered imezindua shindano maalumu la 'Bank more score more', imeelezwa.Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa benki hiyo, Ajmair Riaz alisema lengo la shindano hilo ni kuwafanya wateja wao kufanya miamala ya kibenki kidijitali na kuondokana na mifumo ya kizamani katika kutunza na kutumia fedha zao.

"Katika mwaka huu tunakumbuka ni miaka miwili tangu tuanzishe benki ya kidijitali hapa Tanzania kwa hiyo mwezi huu tunaadhimisha miaka miwili ya mfumo huo,"-alisema Riaz.

Ofisa huyo alisema benki hiyo itatoa zawadi mbalimbali zenye nembo ya Liverpool kama jezi, viatu na mipira ili kuinua ari ya michezo kwa wateja wake na vile vile kusaidia kuimarisha afya."Zawadi nyingine ni kumpeleka Uingereza mshindi ili kutembelea Uwanja wa Anfield uliopo katika jiji la Liverpool na viwanja vingine mbalimbali vya michezo nchini humo pamoja na kukutana na wachezaji wa klabu hiyo," Riaz alisema.

Michezo

Ijumaa Aprili 16, 2021

Nipashe



HABARI UK.22

## Tiketi Ligi ya Mabingwa Ulaya yamvuruga Klopp

# Chambua aipatia Yanga mwarobaini

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa zamani wa Yanga, Sekilojo Chambua, amewataka viongozi wa timu hiyo kubadilisha mfumo wa usajili wa wachezaji wanaoutumia sasa kwa ajili ya kuhakikisha msimu ujao wanapata nyota wenye uwezo mkubwa wa kuitumikia klabu hiyo.

Chambua aliyetamba na Yanga kuanzia katikati ya miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990 aliliambia gazeti hili kwa kubadilisha mfumo wa usajili, klabu hiyo itaingia mikataba na wachezaji wenye tija na uwezo wa kuitumikia timu yao vizuri.

Nyota huyo alisema umefika wakati viongozi na wadhamini wakawatumia watu sahihi ikiwamo wachezaji wa zamani katika kufanikisha mchakato wa usajili na kuachana na njia wanayotumia hivi sasa.

"Viongozi wanatakiwa kufikiri sana kuwa nani anaweza kuwasaidia kupata wachezaji wazuri?. Fedha zipo, wafadhili wapo na wanaonyeshwa na nani wachezaji wazuri ili waende wakasajili? Sisi wachezaji wa zamani mbona tupo lakini hatutumiki? Mimi nipo kwenye Kamati ya Ufundi. Hii inaleta shida namna ambapo hata wachezaji kutoka nje wanavyokuja ni wachezaji, lakini kuna baadhi hawatoshi, hawana uwezo wa kuichezea timu kubwa kama ya Yanga," alisema Chambua.

Nyota huyo ameungana na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, ambaye alisema Yanga ina baadhi ya wachezaji ambao hawajitumi na wengine hawana uwezo na sita ya kuichezea timu hiyo.

Muro ambaye aliwahi kuwa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Yanga alishangazwa kuona timu hiyo kuwa na mastraika ambao wamekaa kipindi cha miezi mitano hadi mwaka bila kufunga bao hata moja na kuongeza Yanga ya sasa siyo kama anayoijua yeye ya 'Kampa Kampa Tena.'

Naye beki wa zamani wa klabu hiyo, Bakari Malima 'Jembe Ulaya' alisema wachezaji wa timu hiyo ndiyo wanaowaangusha viongozi kwa kushindwa kupambana na kupata matokeo chanya.

Alisema anachokiona ni kila siku zinavyozidi kusonga mbele ndiyo viwango vya wachezaji wa Yanga vinaporomoka na kuiweka timu hiyo katika wakati mgumu kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Yanga yenye pointi 51 ndio vinara wa ligi hiyo ikicheza mechi 24 na katika msimamo inafuatiwa na mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 49 lakini imeshuka dimbani mara 21.

# SIMBA: TUMEONYESHA UKUBWA

## ●●● Asema nidhamu ya wachezaji imewabeba huku Kagere akitamba...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, akisema kucheza kwa nidhamu ndio siri iliyochangia timu yake kupata ushindi mnono katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar, kinara wa kupachika mabao, Meddie Kagere, ametangaza amerejea kwa kishindo.



Kiungo wa Simba, Clatous Chama (katikati), akimiliki mpira huku akizongwa na mabeki wa Mtibwa Sugar, Issa Rashid (kushoto) na Abubakar Ame (kulia), katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 5-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Simba ilitoa kipigo kikali cha mabao 5-0 kwa Mtibwa Sugar na kufikisha pointi 49, mbili pungufu dhidi ya vinara wa ligi hiyo, Yanga yenye pointi 51, lakini mabingwa hao watetezi wakiwa na mechi tatu mkononi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gomes alisema anajivunia kuona wachezaji wake wakicheza kwa nidhamu ya hali ya juu katika mchezo huo na kufanikiwa kupata ushindi wa idadi kubwa ya mabao na kujiimarisha kwenye mbio za ubingwa wa msimu huu.

Gomes alisema nyota wake wanafanya kile alichowafundisha katika mazoezi na kila mmoja ametimiza majukumu yake ikiwamo kuwaheshimu wapinzani wao hali ambayo imewasaidia kupata matokeo mazuri katika mchezo huo.

Mfaransa huyo alisema mara kadhaa amekuwa akiwaambia wachezaji wake wanapaswa kuonyesha ukubwa walionao kwa kupata matokeo chanya katika mechi zote za ligi ya nyumbani zilizobakia.

"Niwapongeze wachezaji wangu kwa kupambana na kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu katika mchezo wetu wa leo (juzi), walicheza kwa malengo ya kutafuta matokeo bila kujali tunakutana na timu ambayo iko katika nafasi gani kwenye msimamo, kwetu tulihitaji ushindi ili kufikia malengo yetu ya kuhitaji kutetea ubingwa wetu,".

"Ligi ni ngumu sana na hakuna timu rahisi kwa sababu kila mmoja anahitaji kujinasua katika nafasi aliyokuwapo, aliyekuwa chini anahitaji kupanda juu na wa juu anahitaji kubaki katika nafasi hiyo, hilo tumeliona na tutahakikisha hatutadharau mpinzani yoyote tutakayekutana naye," alisema Gomes.

Alisema kiwango kinachoonyesha wachezaji wake kinaendelea kumpa matumaini makubwa ya kuendelea kufanya vizuri katika mbio za kutetea taji lao la ubingwa ambalo pia linawaniwa na watani zao, Yanga.

Aliongeza wataendelea kujiimarisha na kujipanga na kuyafanyia kazi upungufu mchache uliopo katika kikosi chake kwa ajili ya kwenda kupambana na kupata matokeo mazuri ugenini dhidi ya Mwadui FC, mchezo utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mkoani Shinyanga.

Naye Kagere alisema yuko imara katika vita ya kutetea tuzo ya ufungaji bora anayoishikilia katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaoelekea ukingoni.

Kagere raia wa Rwanda juzi alifunga mabao mawili katika ushindi wa magoli 5-0 na kutimiza idadi ya mabao 11 akifuatiwa na nyota wa Azam FC, Prince Dube mwenye mabao 10 huku John Bocco akiwa wa tatu baada ya kupachika mabao tisa.

Mshambuliaji huyo alisema malengo yake makubwa ni kupambana ili kufikia malengo yake pamoja na kuona Simba inafikia kile inachotarajiwa na wengi.

Naye Kocha wa magolikipa wa Mtibwa Sugar, Soud Slim, alisema timu yake imekubaliana na kichapo ilichopokea na kusema juzi ilikuwa siku ngumu kwao.

Slim alisema benchi la ufundi haliwezi kuwatupia lawama wachezaji wao kutokana na matokeo hao kwa sababu mechi ilikuwa ngumu sana kwao kutokana na Simba kuwa na timu bora na yenye wachezaji wazuri kila idara.

"Ilikuwa siku ngumu kwetu, kwa sababu wachezaji nane walikuwa katika mfungo, siku ya kwanza ya Ramadhan ina wakati mgumu kuizoea, lakini pia Simba ni bora na ina wachezaji imara na wa viwango vya juu kuliko sisi, sasa tunaenda kujipanga kwa ajili ya mechi zijazo ili kutoka katika nafasi tuliyopo ya kujinasua kushuka daraja," alisema Slim.

Mtibwa Sugar yenye pointi 24 iko katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kucheza michezo 24.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >